# UKIUSHI WA KIISIMU KATIKA JUMBE CHESHI ZA MTANDAO

**WANJIRU AGNES WANGECI**

**C50/67042/2013**

**TASNIFU HII INAWASILISHWA KWA MINAJILI YA KUKIDHI BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2018**

## UNGAMO LA MTAHINIWA

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawasilishwa kwa ajili ya shahada yoyote katika chuo kingine chochote.

………………………………………. Date: ……………………

**WANJIRU AGNES WANGECI**

**C50/67042/2013**

UNGAMO LA WASIMAMIZI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi.

…………………………………. Tarehe: ……………………….

**PROFESA IRIBE MWANGI**

………………………………………. Tarehe…………………………

**DAKTARI NYACHAE MICHIRA**

## TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia watoto wangu Ann, Benedict na hasa mtoto Baraka niliyembeba tumboni katika muda wote nilipokuwa nikiifanya kazi hii. Ewe mwanangu mpenzi, u baraka kwa kweli!

## SHUKRANI

Kazi hii imekuwa na changamoto si haba lakini kwa msaada wa wengi nimeweza kuikamilisha. Kwanza namshukuru mwenyezi Mungu kwa kunipa afya tele pamoja na akili timamu iliyojaa hekima. Yote haya yaliniwezesha kufanikisha malengo yangu ya kiusomi hadi kufikia kiwango hiki cha uzamili.

Shukrani za dhati nazitoa kwa wasimamizi wangu Profesa Iribe Mwangi na Daktari Nyachae Michira. Ni kupitia juhudi zao ambapo kazi hii imeweza kukamilika. Shukrani za kipekee zimwendee Profesa Iribe aliyetumia kila njia kunielekeza ikiwemo kujitolea kunipa maelekezo kwa njia ya simu kwa kuwa nilikuwa katika hali ya ujauzito ulioniwia vigumu kusafiri hadi Nairobi kutafuta ushauri wa wasimamizi. Asante kwa kunielewa.

Shukrani pia ziwaendee wahadhiri wote walionifunza kwa mapenzi. Profesa Iribe Mwangi, Profesa Kineene wa Mutiso, Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Prisca Jerono, Dkt Zaja Omboja na wahadhiri wengine wote walionifunza. Nawaombea baraka za Mola.

Pia nawashukuru wasomi wenzangu tulioshirikiana nao, kushauriana na kuhimizana. Wao ni Agnes Muchiri, Winnie Kamau na sahibu Simon Mjomba.

Ninamshukuru kwa moyo wote Bwana Patrick Wangombe wa Kenya Institute of Management (Nyeri) kwa kunifaa sana alipoipanga kazi yangu .

Ninawashukuru wote ambao sikuwataja kwa majina ila walinisaidia kwa njia moja au nyingine. Mungu awajaalie mema daima dawamu.

# YALIYOMO

**UNGAMO LA MTAHINIWA** ..... i
**TABARUKU** ..... ii
**SHUKRANI** ..... iii
**YALIYOMO** ..... iv
**JEDWALI** ..... viii
**MICHORO** ..... ix
**PICHA** ..... x
**MAELEZO YA MSAMIATI** ..... xii
**IKISIRI** ..... xiii
**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ..... 1
1.0 Utangulizi ..... 1
1.0.1 Dhana ya Jumbe cheshi ..... 1
1.0.2 Dhana ya Mtandao ..... 2
1.1 Tatizo la Utafiti ..... 3
1.2 Maswali ya Utafiti ..... 4
1.3 Malengo ya Utafiti ..... 5
1.4 Umuhimu wa Utafiti ..... 5
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti ..... 6
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ..... 7
1.6.1 Dhana ya Mtindo ..... 7
1.6.2 Dhana ya Uchimuzi ..... 8
1.6.3 Ukiushi wa Kiisimu ..... 9
1.6.4 Ukiushi wa Kisarufi ..... 9
1.6.5 Ukiushi wa Kigrafolojia ..... 10
1.6.6 Ukiushi wa Kisemantiki ..... 11
1.6.7 Ukiushi wa Kileksika ..... 12
1.6.8 Ukiushi wa Kisajili ..... 12
1.7 Nadharia za Uhakiki ..... 12
1.7.1 Nadharia ya Semiotiki ..... 13
1.7.2 Nadharia ya Elimu Mitindo ..... 15
1.8 Mbinu za Utafiti ..... 17
1.8.1 Sampuli Kielelezo ..... 17
1.8.2 Mbinu za Ukusanyaji Data ..... 18
**SURA YA PILI: NADHARIA YA JUMBE CHESHI** ..... 20
2.0 Utangulizi ..... 20
2.1 Jumbe Cheshi za Kidijitali ..... 21
2.2 Muundo wa Jumbe Cheshi ..... 22

Picha 1: Muundo wa Jumbe Cheshi ........ 23
Picha 2: Muundo wa Jumbe Cheshi na Maandishi Sehemu ya Chini ........ 23
Picha 3: Muundo wa Jumbe Cheshi bila Picha ........ 23
Picha 4: Muundo wa Jumbe Cheshi na Maandishi katikati mwa Picha ........ 24
Picha 5: Muundo wa Jumbe Cheshi na Picha pekee ........ 24
2.3 Fremu ya Jumbe Cheshi ........ 25
2.4 Jumbe Cheshi Tangazi ........ 26
Picha 7 (a) na (b): Jumbe cheshi Tangazi ........ 26
2.5 Dhana Mfanano ........ 26
2.6 Ucheshi katika Jumbe Cheshi ........ 27
2.8 Muundo kwa kurejelea Muda wa Kudumu ........ 30
2.9 Muundo kwa kurejelea Kiasi cha Mbinu za Kiuandishi kilichotumiwa pamoja na Ukiushi.. 31
2.10 Utata wa Memetiki ........ 31
**SURA YA TATU: UKIUSHI WA KISARUFI KATIKA JUMBE CHESHI** ........ 33
3.0 Utangulizi ........ 33
3.1 Dhana ya Ukawaida na Usanifu wa Lugha ........ 34
3.1.1 Usanifu Nje ........ 34
3.1.2 Usanifu Ndani ........ 35
3.2 Ukiushi wa Kisintaksia katika Jumbe Cheshi ........ 36
3.3 Ukiushi wa Kileksika wa Jumbe Cheshi ........ 37
3.0.1 Uhawilishaji Msimbo ........ 37
Picha 9: Uhawilishaji Msimbo ........ 37
3.3.2 Kuchanganya Ndimi ........ 37
Picha 10: Kuchanganya Ndimi ........ 37
3.3.4 Matumizi ya Lugha Vipindi ........ 37
Picha 11: Matumizi ya Lugha Vipindi ........ 38
3.3.5 Matumizi ya Lafudhi ........ 38
Picha 12 (a) (b) (c): Matumizi ya Lafudhi ........ 39
3.3.6 Utohozi ........ 39
Picha 13: Utohozi ........ 39
3.3.7 Matumizi ya Lugha Bandya za Kisanaa ........ 40
Picha 14: Matumizi ya Lugha Bandya za Kisanaa ........ 40
3.3.8 Uumbaji Maumbo Mapya ........ 40
Picha ya 15; Uumbaji wa maumbo upya ........ 41
3.4 Ukiushi wa Kisintaksia katika Jumbe Cheshi ........ 41
3.4.1 Kishazi ........ 41



Picha 16 (a) na (b): Matumizi ya Vishazi ........ 42

v

3.4.2 Matumizi ya Virai ........ 42
Picha 17 (a) na (b): Matumizi ya Virai ........ 42
3.4.3 Maswali ya Balagha ........ 43
Picha 18 (a) na (b): Maswali ya Balagha ........ 43
3.4.4. Kuboronga Maneno ........ 43
Picha 19: Kuboronga Maneno ........ 44
3.4.4 Sarufi Mvurugo ........ 44
Picha 20: Sarufi Mvurugo ........ 45
3.4.5 Matumizi ya Dayolojia ........ 45
Picha 21: Matumizi ya Dayolojia ........ 45
3.4.6 Usambamba wa Kisintaksia ........ 46
Picha 22: Usambamba katika KT(RT)+KT(RT)+KT(RT)+KT(RT) ........ 46
Picha 23: Usambamba Katika KN1(N)+KT(T+N) +KN2(N)+KT (T+N) ........ 46
Picha 24: Usambamba katika KN1(W)+KT(T+N) +KN2(W)+KT(T+N) ........ 47
3.4.7 Usambamba Kinyume ........ 47
Picha 25: Usambamba Kinyume ........ 47
3.4.8 Usambamba Kimwimo ........ 47
Picha 26: Usambamba Kimwimo ........ 48
3.5 Ukiushi wa kimofolojia ........ 48
3.5.1 Ukatizaji ........ 48
Picha 28: Uambishaji ........ 49
3.5.3 Mnyambuliko ........ 49
Picha 30 (a) na (b): Kitahajia ........ 50
3.5.6 Kuchanganya Maumbo ........ 51
Picha 31: Kuchanganya Maumbo ........ 51
3.5.7 Usambamba wa Kimofolojia ........ 51
Picha 32 (a) na (b): Usambamba wa Kimofolojia ........ 51
**SURA YA NNE: UKIUSHI WA KISAJILI** ........ 52
4.0 Utangulizi ........ 52
Picha 33: Ukiushi wa Kisajili ........ 52
Picha 34: Sajili ya Kibiashara na Siasa ........ 53
Picha 35: Sajili ya kidini ........ 53
Picha 36: Sajili ya darasani kutumiwa kuelezea maswala ya kisiasa ........ 54
Picha 37: Sajili ya kiutawala inatumiwa kuelezea maswala ya kijamii ........ 54
Picha 38 Sajili ya Vijana inatumiwa katika Maongezi ya Mzee ........ 55
4.1 Ukiushi wa Kigrafolojia. ........ 55
Picha 39 (a) na (b): Ukiushi wa Kigrafolojia ........ 55
Picha 40: Matumizi ya Alama za Dukuduku ........ 56
Picha 41: Matumizi ya Herufi Kubwa na Ndogo ........ 56

Picha 42: Alama ya Kinyota kuleta maana ya Mambo yenye Umarufuku ................................. 57
Picha 43: Maandishi yanayodhihiri maana kulingana na Sehemu yalikowekwa ........................ 57
Picha 44: Kundi la Jumbe Cheshi Kadha katika Ukurasa Mmoja .............................................. 58
4.2 Ukiushi wa Kisemantiki............................................................................................... 59
Picha 46: Matumizi ya Sitiari.......................................................................................... 59
Picha 47: Matumizi ya Tashbihi ...................................................................................... 60
Picha 49 (a) na (b): Matumizi ya Kinaya .......................................................................... 61
**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ............................ 62
5.0 Utangulizi..................................................................................................................... 62
5.1 Muhtasari ..................................................................................................................... 62
5.2 Changamoto katika Utafiti ........................................................................................... 63
5.3 Mapendekezo ............................................................................................................... 64
**MAREJELEO** ............................................................................................................... 65

## JEDWALI

Jedwali 1. Jedwali la fomula ya sampuli kielelezo ........................................................................ 18

## MICHORO

Mchoro 1: Mduara wa Kifolololojia ........................................................................................ 8
Mchoro 2: Dhana ya Uchimuzi ............................................................................................... 9
Mchoro 3: Uhusiano wa Ishara Kulingana na Pierce (1991) ........................................................ 13

## PICHA

Picha 1: Muundo Wa Jumbe Cheshi ........ 23
Picha 2: Muundo wa Jumbe Cheshi na Maandishi Sehemu ya Chini ........ 23
Picha 3: Muundo wa Jumbe Cheshi bila Picha ........ 23
Picha 4: Muundo wa Jumbe Cheshi na Maandishi Katikati mwa Picha ........ 24
Picha 5: Muundo wa Jumbe Cheshi na Picha Pekee ........ 24
Picha 6 (a) na (b): Jumbe Cheshi Zinazowatumia Wahusika Maarufu Kama Fremu ........ 25
Picha 7 (a) na (b): Jumbe cheshi tangazi ........ 26
Picha 9: Uhawilishaji Msimbo ........ 37
Picha 10: Kuchanganya Ndimi ........ 37
Picha 11: Matumizi ya Lugha Vipindi ........ 38
Picha 12 (a) (b) (c): Matumizi ya Lafudhi ........ 39
Picha 13: Utohozi ........ 39
Picha 14: Matumizi ya Lugha Bandya za Kisanaa ........ 40
Picha ya 15; uumbaji wa maumbo upya ........ 41
Picha 16 (a) na (b): Matumizi ya Vishazi ........ 42
Picha 17 (a) na (b): Matumizi ya Virai ........ 42
Picha 18 (a) na (b): Maswali ya Balagha ........ 43
Picha 19: kuboronga maneno ........ 44
Picha 20: Sarufi Mvurugo ........ 45
Picha 21: Matumizi ya Dayolojia ........ 45
Picha 22: Usambamba Katika KT(RT)+KT(RT)+KT(RT)+KT(RT) ........ 46
Picha 23: Usambamba Katika KN1(N)+KT(T+N) +KN2(N)+KT (T+N) ........ 46
Picha 24: Usambamba Katika KN1(W)+KT(T+N) +KN2(W)+KT(T+N) ........ 47
Picha 25: Usambamba Kinyume ........ 47
Picha 26: Usambamba Kimwimo ........ 48
Picha 27: Ukatizaji ........ 48
Picha 28: Uambishaji ........ 49
Picha 30 (a) na (b): Kitahajia ........ 50
Picha 31: Kuchanganya Maumbo ........ 51
Picha 32 (a) na (b): Usambamba wa Kimofolojia ........ 51
Picha 33: Ukiushi wa Kisajili ........ 52
Picha 34: Sajili ya Kibiashara na Siasa ........ 53
Picha 35: Sajili ya kidini ........ 53

Picha 36: Sajili ya darasani kutumiwa kuelezea maswala ya kisiasa........................................... 54
Picha 37: Sajili ya kiutawala inatumiwa kuelezea maswala ya kijamii...................................... 54
Picha 38 Sajili ya vijana inatumiwa katika maongezi ya mzee ................................................... 55
Picha 39 (a) na (b): Ukiushi wa Kigrafolojia ................................................................................ 55
Picha 40: Matumizi ya Alama za Dukuduku .................................................................................. 56
Picha 41: Matumizi ya herufi kubwa na ndogo ............................................................................. 56
Picha 42: Alama ya kinyota kuleta maana ya mambo yenye umarufuku .................................... 57
Picha 43: Maandishi yanayodhihiri maana kulingana na sehemu yaliyowekwa .......................... 57
Picha 44: Kundijumbe Cheshi kadha katika Ukurasa Mmoja ...................................................... 58
Picha 45: Kutoakifisha sentensi ...................................................................................................... 58
Picha 46: Matumizi ya Sitiari........................................................................................................... 59
Picha 47: Matumizi ya tashbihi........................................................................................................ 60
Picha 48: Matumizi ya Chuku........................................................................................................... 60
Picha 49 (a) na (b): Matumizi ya kinaya......................................................................................... 61

## MAELEZO YA MSAMIATI

| | |
|---|---|
| **Jumbe Cheshi** | Picha, video au ujumbe maandishi ambao kwa kawaida huwa wenye ucheshi. Hunakilishwa na kusambazwa kwa kasi miongoni mwa watumizi mtandao huku ukifanyiwa mabadiliko machache wakati mwingine. |

# IKISIRI

Utafiti wetu ulilenga kuonyesha ukiushi wa kiisimu katika jumbe cheshi za mtandao katika viwango sita ambavyo ni kiwango cha kigrafolojia, kilekska, kimofolojia, kisintaksia, kisajili na pia kisemantiki. Kwa kuonyesha ukiushi wa kiisimu katika jumbe cheshi, tulilenga kupinga kwa njia moja fikra kuzihusu jumbe cheshi kuwa zinajitokeza na makosa ya aina mbalimbali kama vile ya kisarufi. Kwa hivyo, tulidhibitisha katika utafiti wetu kuwa ukiushi wa kiisimu haujajitokeza kimakosa bali ni tukio la kimakusudi linalolenga kuongezea mvuto wa kiusanii kwenye akili ya msomaji ujumbe. Tuliongozwa na nadharia mbili ambazo ni nadharia ya semiotiki inayohusu ishara za lugha na pia nadharia ya elimumitindo inayohusu ufafanuzi wa kiisimu kuhusu mitindo mbalimbali inayojitokeza katika matini mbalimbali za kisanii. Jumbe cheshi ambazo ndizo data ya uchunguzi zimesakuriwa kutoka kwa wavuti mbalimbali na husambazwa kupitia mtandao kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Jumbe cheshi hizi zilichanganuliwa na matokeo yake yalirekodiwa katika sura ya tatu na ya nne. Idadi ya jumbe cheshi 49 zilitumika kama data ya uchunguzi. Matokeo ya utafiti yalidhibitisha ukiushi wa kiisimu wa jumbe cheshi za mtandao katika viwango vilivyotajwa.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Mitandao ya kijamii mintarafu Facebook, Whatsapp, Twitter, Instagramu imesababisha mawasiliano kwa namna yake miongoni mwa watu wa matabaka mbalimbali. Jumbe katika mitandao ni za aina tofauti. Kuna jumbe zinazowasilishwa kwa njia ya video, nyingine ni za picha tu bila kuambatanishwa na maelezo au maandishi. Maana zake hubainishwa kwa kuchanganua picha yenyewe kama inavyojitokeza. Jumbe nyingine za mitandao hujitokeza kama vijipicha ambavyo hubeba maana toauti tofauti. Vilevile kuna jumbe zinazoambatanisha picha pamoja na jumbe za maandishi.

Maneno hunuiwa kuifafanua maana za ile picha husika kwa undani. Isitoshe, kuna jumbe za kimaandishi zinazopigwa taipu na kutumwa kwa lengo la kuwasiliana miongoni mwa watumizi mitandao. Jumbe hizi huwa zenye ubinafsi au wakati mwingine huru. Jumbe za kibinafsi hutumwa kwa watu waliokusudiwa lakini zile huru hutumwa kiholela na kusambazwa kwa wanaofurahia huduma za mtandao. Pia kuna jumbe zinazosheheni maana yake kwa kusikiza maneno yaliyorekodiwa. Utafiti huu utajikita kuchanganua jumbe cheshi zinazojitokeza kwa mtindo wa picha zinazoambatanishwa na jumbe maandishi. Aidha, uchanganuzi wetu utahusisha jumbe zinazojitokeza kwa maandishi katika lugha ya Kiswahili pekee na pia jumbe zinazochanganya msimbo kimaandishi.

### 1.0.1 Dhana ya Jumbe cheshi

Neno "jumbe cheshi" limetafsiriwa kutoka kwa neno katika lugha ya Kiingereza "meme" ambapo matamshi yake sahihi katika fonolojia ya Kiingereza ni /miim/ na tafsiri yake katika lugha ya Kiswahili litakuwa "jumbe cheshi". Kulingana na Shifman (2013), jumbe cheshi ni fikra, ucheshi ama dhana zinazosambazwa kwenye mitandao bila vizuizi vyovyote. Jumbe cheshi hizi huwa katika maumbo ya picha, video au muziki. Jumbe cheshi ni mchoro, picha, video au maandishi fulani ambayo kwa kawaida huzua ucheshi na hutayarishwa na kisha husambazwa harakaharaka kupitia mtandao kwa wanaotumia huduma za mitandao ya kijamii.

Kulingana na Paul Gil (2016), jumbe cheshi ni wazo, tabia au mtindo ambao husambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine katika utamaduni mmoja kwa lengo la kuwasilisha jambo fulani, maudhui au maana inayofumbatwa na huo ujumbe cheshi. Anaeleza kuwa

jumbe cheshi ni ishara au dhana za kijamii. Neno “meme” liliasisiwa na mwanabayolojia kwa jina Dawkin (1976) aliuhusisha mchakato wa namna chembechembe za uzazi zinavyosambazwa kutoka kiini chake hadi kwa kiumbe mwingine na namna jumbe cheshi zinavyosambazwa haraka kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Blackmore (2001) na Gil (2016) ni miongoni mwa watu walioyaunga mkono mawazo ya Dawkin. Waliziona jumbe cheshi kama viungo vyenye uhai namna tu chembechembe za kizazi zilivyo na uhai wa kurithisha kizazi. Kwamba jumbe cheshi huwa na uwezo wa kuigwa mara nyingi iwezekanavyo zinapopitisha sifa fulani za kibinadamu. Jumbe cheshi hupitisha maswala ya kitamaduni kama vile lugha, desturi, mitindo ya ulaji n.k. Nyingi ya jumbe cheshi katika ulimwengu wa sasa huwa vijipicha ambavyo huzua vicheko kwa lengo la kuzua tashtiti ili kukejeli tabia za binadamu. Jumbe cheshi zingine huweza kuwa video au jumbe cheshi za kisauti.Jumbe cheshi zingine huwasilisha mawazo mazito na yenye hekima ya kiwango cha juu sana. Jumbe cheshi hutegemea mashine kama tarakilishi au simu ya mkononi ili kusambazwa. Huu ni mfumo wa mawasiliano ambao ni mwepesi na umeshika kasi sana katika jamii ya leo.

### 1.0.2 Dhana ya Mtandao

Mtandao ni njia maalum ya kuwaunganisha watu katika enzi hii ya kidijitali. Taarifa za kila aina kutoka ulimwengu wote huweza kuwasilishwa kupitia mtandao. Taarifa zinazowasilishwa ni pamoja na picha mbalimbali, video, taarifa za tafiti, habari zinazochipuka miongoni mwa taarifa nyinginezo. Mtandao pia huwawezesha watu mbalimbali kutangamana kwa sababu mbalimbali kama vile za kibiashara, kirafiki n.k. Mawasiliano hayo huwezeshwa kwa matumizi ya tarakilishi na pia smatifoni. Mashine hizi huwawezesha watu kutangamana kwa kuwasiliana kwa malengo mbalimbali. Jumbe cheshi za mtandao ndizo data yetu ya kiuchanganuzi na data hiyo itachotwa kupitia kwa mtandao. Tunatarajia kuipata data yetu kutoka kwa wavuti mbalimbali ambazo ni wazi kwa yeyote bora awe na tarakilishi au smatifoni na pia aweze kuitumia huduma hii ya mtandao.

Mitindo anuwai ya kiisimu hujitokeza katika miundo ya lugha inayojitokeza katika jumbe hizi. Mitindo hii huwezesha mawasiliano kufanyika huku ikiwafanya wasomaji kuathirika kwa namna mbalimbali kihisia. Tuliaangazia swala la ukiushi wa kiisimu kama unavyojitokeza kama mtindo wa jumbe cheshi za mtandao. Tatizo letu lina msingi wake kwenye ukweli kwamba, lugha ya maandishi hudhibitiwa na sheria pamoja na kanuni mbalimbali kuliko lugha ya kusemwa katika miundo yake. Lugha ya maandishi huwakilisha

lugha sanifu kisarufi. Lugha ya kusemwa kwa kawaida hudhihirisha lugha isiyo sanifu wala dhabiti. Jukumu la lugha ya kimaandishi ni kusaidia katika ufafanuzi wa kiisimu na kwa hivyo lugha ya maandishi kila mara hukumbana na uchanganuzi wa kisayansi. Pia, kauli zozote za kiuchanganuzi wa kisayansi zinastahili kutokana na lugha ya kimaandishi.

Hata ingawa mtandao una manufaa mengi kwa watumizi wake, pia kuna athari hasi zinazohusishwa na matumizi ya mtandao. Yebonah na Dominic (2014), walichanganua athari za matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo huko nchini Ghana. Uchunguzi wao ulionyesha athari hasi za jumbe za mitandao miongoni mwa wanafunzi. Kwamba husababisha upotevu mwingi wa wakati wa kusoma na husababisha wanafunzi kuwa na makosa mengi katika uundaji wao wa sentensi. Pia huwafanya wanafunzi kutofuata ratiba zao za masomo na kwa hivyo kuzembea masomoni mwao kwa kukosa uzingativu.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Utafiti wetu unajikita katika kuchanganua jumbe cheshi zinazotumwa kupitia mitandao ya kijamii asili yake ikiwa kutoka kwa wavuti mbalimbali. Uvumbuzi wa kiteknolojia kila mara hutuelekeza kuvumbua maswala mapya ya kiutamaduni. Hii ni kwa sababu jumbe cheshi kama tokeo la kiteknolojia huonyesha mtindo maalum katika kuwasiliana kwake. Katika kila jamii, lugha ya kimaandishi hupewa hadhi ya juu na mwanadamu na hutumiwa kama kigezo cha urejelezi na binadamu. Maandishi ya lugha iliyosanifishwa ndiyo msingi wa kufafanua ukawaida wa lugha. Lugha hiyo iliyosanifishwa kwa kawaida huchukuliwa kama ndiyo sahihi katika kiwango cha kiisimu. Maandishi yoyote yale hubeba udhabiti na uwajibikaji ambao huchukuliwa kuwa sahihi kama waraka kielelezo cha kusuluhisha matatizo mbalimbali ya lugha. Lugha ya Kiswahili kama lugha iliyosanifishwa inafafanuliwa na kanuni na sheria za lugha katika kiwango cha kiisimu.

Jumbe cheshi tunazochanganua zinahusisha jumbe maandishi. Maandishi ya jumbe cheshi hizi kwa kutumia vigezo vya kupimia lugha sanifu yanaonekana kukiuka kaida za lugha sanifu. Tunapochunguza jumbe cheshi kwa jumla, picha ya kwanza tunayopata kuzihusu ni makosa tofauti tofauti yaliyomo katika jumbemaandishi za jumbe cheshi. Makosa hayo yanayoonekana wazi ni ya kisarufi, ya kitahajia miongoni mwa mengine mengi ambayo kwa mujibu wa lugha sanifu, tunaweza kusema kuwa jumbe hizo zinakosa usahihi. Tunayarejelea kama makosa kwa kuwa yanaonyesha hali tofauti na kanuni za lugha ya Kiswahili sanifu. Burt na Kiparsky (1972) katika uhakiki wa makosa ya mtumizilugha wanatambua aina mbili za makosa ambazo ni makosa ya kawaida na makosa makuu. Kulingana nao, makosa haya

huchipuka katika upokezi wa lugha ya pili na mtu binafsi au katika uhamishaji lugha. Makosa haya wanasema kuwa hudhihirika katika viwango vyote vya lugha. Katika kufafanua tatizo letu la utafiti, maoni yetu ni kuwa jumbe cheshi hazina makosa yoyote ya lugha na kwamba jumbe zenyewe zina usahihi wake maalum. Kinachoonekana na kurejelewa kama makosa ni ukiushi mbalimbali wa kiisimu katika viwango tofauti vya lugha.

Ukiushi huo ni swala la kisanii na unajitokeza kimakusudi katika jumbe cheshi ili kumfanya msomaji alione jambo fulani kwa uwazi zaidi. Makosa huzua hali ya usahihi na kutokuwa sahihi kwa ujumbehusika. Kwa mawazo haya, tunalenga kudhibitisha kuwa jumbe cheshi tunazonuia kuchanganua zina usahihi wa lugha na kinachojitokeza ni hali mbalimbali za ukiushi wa kiisimu ili kuweza kuafikia mvuto wa kiusanii kwa msomaji. Aidha, maneno katika jumbe hizi huambatana na picha ambazo huzua hisia mbalimbali kwa namna maalum. Picha hizi pamoja na maneno hukamilishana ili kuwasilisha maana mbalimbali. Mitindo hiyo mbalimbali ya kiisimu kwenye maandishi na picha hunuiwa kuleta athari kwa mpokea ujumbe na kwa njia hii kuzua maana ambazo ni zaidi na iliyo wazi. Ni katika wazo hili ndipo tulipopata tatizo letu la utafiti.

Wachanganuzi mbalimbali wamekuwa wakichanganua na kuhakiki matini mbalimbali kwa kufuata mwelekeo wa kiisimu. Hakuna kazi yoyote iliyotafitiwa ili kuchanganua maswala ya ukiushi wa kiisimu wa jumbe cheshi za mtandao. Aidha, swala la ukiushi linahusishwa kwa kiwango kikubwa na matini za kishairi. Aidha, hata ingawa tafiti kuhusu lugha na matumizi ya mtandao zimefanywa, hakuna utafiti wowote uliofanywa kuhusu mchango na umuhimu wa jumbe cheshi katika jamii. Pia, swala la jukumu na nafasi ya jumbe cheshi katika lugha pamoja na utendakazi wake katika mawasiliano katika jamii husus an katika nchi ya Kenya halijafanyiwa utafiti wowote. Ni katika wazo hili ndipo tulipopata pengo letu la kufanyia utafiti.

## 1.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti wetu utayafafanua wazi maswala yafuatayo:

a) Ni kwa njia gani ambavyo jumbe cheshi za mtandao huonyesha ukiushi wa kiisimu katika kiwango cha kigrafolojia?

b) Jumbe cheshi hizi hudhihirisha ukiushi katika kiwango cha kisarufi kupitia miundo ipi ya sentensi?

c) Jumbe cheshi hizi hudhihirisha ukiushi katika kiwango cha kileksika kupitia maumbo yapi ya maneno?

d) Jumbe cheshi hizi hujitokeza kama ishara zenye maana kwa kukiuka kanuni zipi za kiisimu katika kiwango cha kisemantiki?

e) Ukiushi wa kisajili hujitokeza kwa njia zipi katika jumbe jumbe cheshi za mtandao?

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti wetu unalenga;

(a) Kuchanganua ukiushi wa kigrafolojia kama unavyojitokeza katika jumbe jumbe cheshi za mtandao.

(b) Kuonyesha ukiushi wa kileksika kama unavyojitokeza katika jumbe cheshi za mtandao.

(c) Kuchanganua ukiushi wa kisarufi katika jumbe cheshi za mtandao.

(d) Kufafanua namna jumbe cheshi za mtandao zinavyoonyesha ukiushi wa kisajili katika uwasilishaji wake.

(e) Kudhibitisha kuwa jumbe cheshi zina ukiushi katika kiwango cha kisemantiki na kwa hivyo zinaonyesha maana mbalimbali kama zilivyokusudiwa.

### 1.4 Umuhimu wa Utafiti

Wasomi wa kazi yetu wataona kuwa kanuni hizi za kisarufi katika jumbe cheshi hukiukwa kimakusudi kwa lengo la kuunda mvuto wa kiusanii katika matini husika. Freeman (1970) anasema kuwa ukiukaji wa kanuni katika mfumolugha ndiyo sababu kuu inayozalisha lugha ya kisanii na bila ukiukaji wa kanuni hakungekuwa na matini za kisanii. Katika kuyaunga mkono mawazo ya Freeman, tumeonyesha namna jumbe cheshi zinavyokiuka kanuni za kiisimu na kwamba bila ukiukaji huu haziwezi kuitika jina jumbe cheshi. Kazi yetu itatolewa kwa manufaa ya wanafunzi na watafiti.

Matokeo ya utafiti wetu utawafaa wahusika mbalimbali katika jamii wakiwemo wasomi na wataalamu wa lugha, mashirika mbalimbali ya kimawasiliano na ya kiserikali, waundaji

programu za mtandao zinazotumia smatifoni na vifaa vya kielektroniki kama vile tarakilishi bila kuwasahau wanajamii mbalimbali kwa jumla.

## 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Tunalenga kuchanganua swala la ukiushi wa kiisimu kama dhana kuu ya kiuchimuzi katika jumbe cheshi za mtandao. Tutalichanganua swala hili kwa mwelekeo wa kiisimumitindo. Utafiti wetu unalenga kuonyesha ukiushi wa kiisimu huku tukikipuuza kiwango cha kifonolojia kwa kuwa utafiti wetu unahusisha dhana za kimaandishi. Hii ni kwa sababu sarufi inahusu uundaji wa sentensi (sintaksia). Sintaksia inahusu mpangilio wa maneno. Hii ina maana kuwa hatuwezi kutenganisha dhana ya maneno(mofolojia) na uundaji wa sentensi. Kwa wazo hili, tunalenga kuchanganua maswala ya ukiushi wa kisintaksia na yale ya kimofolojia. Maswala ya kisintaksia ni kama vile udondoshaji, anafora, epifora kama dhana mbalimbali za urudiaji miongoni mwa dhana nyingine za kisintaksia kama zinavyojitokeza katika jumbe cheshi. Pili, tutachanganua maswala ya ukiushi wa kimofolojia kama yanavyojitokeza katika jumbe cheshi hizi.

Ukiushi wa kimofolojia unahusu miundo tofauti ya maneno ambayo yanakiuka mifumo ya kawaida ya uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. Pia, tutachanganua swala la grafolojia kama linavyojitokeza katika jumbe cheshi. Grafolojia inahusiana na tahajia, uakifishaji pamoja na maswala yote yanayohusiana na grafiki katika maandishi ya jumbe cheshi. Vilevile, swala la uundaji wa msamiati hujitokeza katika jumbe cheshi tunapopata maneno mapya yaliyoundwa kwa namna tofauti kwenye jumbe cheshi. Ukiushi wa kileksika kama unavyojitokeza katika jumbe cheshi utachanganuliwa. Aidha kuna ukiushi wa kisemantiki kama unavyojitokeza katika jumbe cheshi. Tutalenga kuonyesha namna maana kiisimu inavyosimbuliwa kupitia jumbe cheshi za mtandao kupitia njia kama vile oksimora, tautolojia miongoni mwa mitindo mingine. Jumbe cheshi tutakazotumia kama data ni zile zinazotumia lugha ya Kiswahili pekee au zinazochanganya msimbo huku lugha ya Kiswahili ikijitokeza kama lugha kuu katika jumbe cheshi hizo.

Data itachotwa kwa wavuti kama zifuatazo: Nairobiwire.com, Facebook.com, Mpasho.co.ke, trendkenyaonlineblogs, Youthvillage.co.ke, Funnyton.com, Kiss100.co.ke, Classic105.com, na Kenya crazymedias. Utafiti huu utajifunga kwenye malengo yake matatu makuu na utafanywa kwa kipindi cha miezi kumi (kutoka mwezi wa Januari hadi Oktoba mwaka 2018)


## 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

### 1.6.1 Dhana ya Mtindo

Kulingana na Thornborrow na Wareings (1998), uchanganuzi wa isimumitindo hufanywa katika viwango vya kisintaksia, kimofolojia, kileksika, kisemantiki na pia kigrafolojia/kifonolojia. Kwamba lengo kuu la wasomi ni kutambua sifa za kiusanii pamoja na kuchanganua miundo ya kiisimu ya matini mbalimbali, kwa mfano, ukiushi wa kiuakifishaji unaweza kudokeza maana fulani kama vile mfululizo wa vitendo fulani kutokea. Matumizi ya mshangao waweza kuleta maana ya mshtuko au kufa moyo baada ya kutamauka n.k**.** Mtindo unahusiana na parole. Kulingana na Murry (1976) mtindo ni ubora wa lugha katika kueleza hisia fulani au fikira fulani kulingana na mwandishi au msemaji.

Mukarovsky (1964:18) anaeleza mtindo kama ukiushi wa kanuni fulani. Ukiushi huu hujitokeza katika mpangilio wa sauti, maneno au sentensi. Kwa maoni yetu mtindo ni ruwaza fulani zinazojirudiarudia kama sifa fulani katika lugha. Ni namna ambavyo virai, vishazi, sentensi huundwa kwa mitindo fulani. Ufafanuzi wetu unatokana na maelezo ya Chapman (1973) anayeeleza kuwa matini fulani huonyesha uchaguzi na ruwaza za vigezo fulani zinazoleta athari inayokusudiwa. Kwa mujibu wa Leech (1969), kuna uhusiano uliopo baina ya mtindo na mwandishi. Haya yanarejelea utubinafsi wake. Haya ni kwa mujibu wa tamko la kilatini "stilus virum arguit" kwa maana kuwa mtindo humtangaza binadamu.

Elimumitindo ni uwanja unaotathmini sifa za kiisimu katika matini. Kwamba kuna uhusiano baina ya lugha na uamilifu wake wa kisanii. Swala la mwongozo hapa sio nini, kwa nini au kwa jinsi gani bali ni kujiuliza ni kwa sababu gani mwandishi huteua kujieleza kwa njia fulani. Mambo mawili muhimu hapa ni mvuto wa kisanii na uisimu. Spitzer (1967) ametumia mduara wa kifolololojia kufafanua haya. Kwamba mtazamo wa kiisimumitindo huathiri zaidi mitazamo ya kiuandishi nayo mitazamo ya kiuandishi huathiri mitazamo ya kiisimumitindo. Mtindo ni namna ya kujieleza kwa namna mtu anavyoyapanga mawazo yake. Mtindo unaweza kuelezwa kama namna ya kuandika. Mduara huo unaonyeshwa hapa chini.



**Mchoro 1: Mduara wa Kifololojia kulingana na Spitzer (1967)**


### 1.6.2 Dhana ya Uchimuzi

Dhana hii iliasisiwa na wanaisimu wa shule ya Prague. Dhana hii ilitumiwa kueleza sifa za lugha ya kishairi ambayo ilionekana kuwa tofauti na aina zingine zote za mitindo ya kiuandishi. Wanaprague walirejelea uchimuzi kama "aktualisce" kwa maana ya kuchimuza. Mukarovsky (1964) anaeleza uchimuzi kama ukiukaji kimakusudi wa kanuni katika lugha sanifu. Kwamba ni uwezo wa kuzikiuka kanuni kwa lengo la kuunda mvuto wa kiusanii katika matinihusika. Kwa mujibu wa Freeman (1970) uchimuzi unahusiana na ukiushi na swala la ukiushi linahusiana na uchimuzi pia. Leech (1969) anaeleza uchimuzi kama ukiushi wa kimakusudi wa kanuni za msimbo wa lugha ama kwenda kinyume na matumizi ya lugha yaliyokubalika. Ni lugha kuchimuzwa mbali na matumizi yake ya kawaida.

Fowler (1973) anaeleza uchimuzi kama unaohusiana zaidi na ukiushi wa kiisimu. Ni ukiukaji wa kanuni ambao hufanywa na mshairi na ambao humzindua msomaji akahama kutoka maelezo yaliyofinyangwa hadi kwa kiwango kingine cha uelewa. Leech na Short (1981) wanaeleza uchimuzi kama ukiushi unaosababishwa na maswala ya kisanii. Kulingana nao, uchimuzi ni jumla ya mitindo ya kiisimu inayojitokeza katika matini mbalimbali. Kujitokeza huku huwa ni katika viwango vya kifonetiki, kisarufi, kisematiki n.k. Uchimuzi hufikiwa kupitia kwa njia mbili ambazo ni; ukiushi na usambamba. Uchimuzi ni namna maalum ya kueleza wazo au jambo kwa njia wazi kwa kuifanya kazi ya sanaa kuvutia macho. Uchimuzi huweza kuafikiwa katika viwango vyote vya kiisimu. Kwa mfano, katika kiwango cha kisarufi, kuna udondoshi ambapo muundo wa sentensi huwa hauna kiima au kiarifa ama vyote viwili. Sehemu hii hudondolewa na mzungumzaji kimakusudi kwa sababu za kimawasiliano au labda anapotaka kuokoa muda wake.

Matokeo ya uchimuzi ni kulikuza jambo katika kazi ya sanaa na kulifanya litokeze kiasi cha kumvutia msomaji. Uchimuzi unaajinabisha miundo ya lugha ya kawaida. Uchimuzi hurejelea sifa zozote za kiisimu zinazotumiwa kumfanya msomaji alione jambo fulani kwa uwazi zaidi. Uchimuzi unahusu muundo ambao utajitokeza mara kwa mara na pia kwa mfuatano fulani kimkweo. Haya ni kulingana na Leech. Kwamba panaweza kuwa na mpangilio fulani wa urudiaji silabi au sitiari zinazohusiana. Sifa moja kuu itaonekana kutawala zaidi kuliko sifa nyinginezo. Miall na Kuiken (1994) wanairejelea dhana ya uchimuzi kama tofauti za kimtindo ambazo huamsha hisia mbalimbali na kujenga taharuki. Kwamba kuna ushahidi kuwa uchimuzi katika matini za kifasihi huwafanya wasomaji

kuvutiwa na pia nadhari zao hutekwa. Leech na Short (1981) walifasiri uchimuzi kama dhana inayohusisha vigezo viwili kama ifuatavyo:




**Mchoro 2: Dhana ya Uchimuzi kwa mujibu wa Leech na Short (1981)**

### 1.6.3 Ukiushi wa Kiisimu

Wakati mwandishi anapotaka lugha yake ionekane bunifu, hutumia lugha kwa namna tofauti na matumizi ya kawaida ya lugha hiyo. Jambo hili huathiri msomaji wake hivi kwamba anakuja kustaajabia kazi hiyo. Namna hii maalum ya kutumia lugha kwa njia maalum hurejelewa kama ukiushi wa kiisimu. Leech (1969) anasema kuwa,

> "Yeyote anayetarajia kuonyesha ubora wa kazi ya usanii ni lazima atilie muhimu kuajanabisha na kuathiri kwa namna maalum akili ya msomaji wake. Ukiushi huu wa kiisimu uliokubalika unarejelewa kama uchimuzi."

Leech anaangazia aina nane tofauti za ukiushi wa kiisimu. Aina hizi amezichota kutokana na viwango vitatu vikuu vya lugha ambavyo ni; Uelewekaji; Umbo; na Semantiki.Uelewekaji hudhihirika katika kiwango cha kifonolojia na kigrafolojia. Umbo huhusisha sarufi na uleksika nacho kiwango cha semantiki hurejelea maana tambuzi. Ni muhimu kutambua kuwa Leech anaangazia vigezo hivi akirejelea kazi ya ushairi lakini kwa maoni yetu mwelekeo wake unaweza kutumiwa kufafanua kazi zozote za kisanii za kimaandishi zikiwemo jumbe cheshi tunazochanganua. Tutaangazia aina tano za ukiushi wa kiisimu tukitumia jumbe cheshi kama kigezo chetu cha kiuchambuzi. Tutajifunga katika kufafanua aina tano za ukiushi wa kiisimu katika jumbe cheshi ambazo ni; ukiushi wa kigrafolojia, ukiushi wa kileksika, ukiushi wa kisarufi (mofolojia na sintaksia), ukiushi wa kisemantiki na ukiushi wa kisajili.

### 1.6.4 Ukiushi wa Kisarufi

Ukiushi una maana ya ukiukaji wa kanuni ambazo hufuatwa kwa kawaida. Ni namna ya kuepuka kanuni ya kawaida iliyozoeleka kwa mfano kanuni ya kisarufi iliyozoeleka ya kupanga maneno kwa namna maalum katika sentensi inaweza kukiukwa katika matini fulani. Ukiushi huhusisha uteuzi wa kiisimu wa kibinafsi. Ukiushi unahusisha maana ya kazi na

tathmini ya kisanii inayohusishwa na ufafanuzi maana. Mwandishi anaweza kuyaendeleza maneno kwa jinsi tofauti au atumie msamiati usiokuwa wa kawaida miongoni mwa mambo mengineyo. Ukiushi hujitokeza katika viwango mbalimbali vya lugha kama vile vya kimaandishi, kisauti, kisemantiki, kisajili, au pia katika kukiuka awamu za kihistoria.

Mada yetu inalenga kufafanua ukiushi wa kiisimu katika jumbe cheshi za mitandao. Ukiushi wa kisarufi hudhihirika katika miundo ya kimofolojia ya maneno na katika mipangilio ya maneno katika sentensi (sintaksia). Kulingana na Habwe na Karanja (2003), wanasarufi mapokeo walifanya uchunguzi kuhusu sarufi ya lugha. Kulingana na uchunguzi huo wa wanasarufi mapokeo, sintaksia ni sehemu ya sarufi ya lugha inayojumlisha pia mofolojia na kwa kiwango fulani fonolojia. Sarufi ina maana ya "usahihi" unaohusishwa na sanaa ya maandishi na wenye mfumo wa sheria za matumizi ya lugha. Sarufi ni utaratibu wa kanuni zinazomwezesha mtumizi lugha kutoa tungo sahihi ili zieleweke zinapotolewa pia na mtu mwingine. Mtazamo huu unaonyesha kuwa kuna sarufi sahihi na isiyo sahihi.

Katika utafiti wetu, tutalenga kuonyesha miundo ya kimofolojia na ya kisintaksia ambayo si ya kawaida kulingana na sarufi ya lugha ya Kiswahili. Ukiushi huu wa kisarufi utachanganuliwa kama unavyojitokeza katika jumbe cheshi za mtandao. Maswala ya kisintaksia ambayo hudhihirisha ukiushi ni pamoja na kukiuka kanuni za kisarufi katika mvurugo wa mpangilio wa maneno katika sentensi, miundo tofauti ya sentensi n.k. Kulingana na Leech na Short (1981) ukiushi wa kimofolojia unahusu kuelezea maswala ya ukiukaji katika namna maneno yanavyoundwa,maumbo ya maneno yasiyo ya kawaida kwa mujibu wa lugha ya Kiswahili, mnyambuliko usio sahihi miongoni mwa maswala mengine ya kimofolojia. Kulingana nao, ukiushi hujitokeza kwenye misimbo ya lugha. Vilevile, ukiushi una athari chanya na hasi kwa upande mwingine. Sifa hii hujitokeza kama ruwaza za kimaandishi ambapo matini fulani inaweza kujiamulia kanuni zake kando na zile za kawaida. Matini hiyo huweza kujitenga na ikawa tofauti na namna matini hiyo inavyostahili kuwa. Kwa mfano, kutumia mtindo wa kishairi katika kazi za kinathari. Chapman (1973) anaeleza ukiushi wa kileksika, kisintaksia au kifonolojia kama dhana zisizojitokeza kwa kiasi kikubwa katika matini. Aliuita "unadra" kwa maana kuwa mwandishi hujizulia muundo wa ruwaza fulani unaosababisha ukiushi wa aina fulani.

### 1.6.5 Ukiushi wa Kigrafolojia

Grafolojia ni uchanganuzi wa kiisimu unaohusisha kuchanganua maswala ya kigrafiki katika lugha. Tawi hili liliasisiwa katika isimu ya lugha katika miaka ya sitini na Mcintosh (1960).

Alihusisha grafolojia na lugha ya maandishi na namna tunavyohusisha fonolojia na lugha ya kusemwa. Baadaye, mawazo yake yaliendelezwa na Halliday & Strevens (1964). Walihusisha grafolojia na tahajia, uakifishaji na, maswala yote yanayohusishwa na grafiki katika lugha. Wengine walioendeleza nadharia hii ni Vachek (1973), Sampson (1985), Coulmas (1991) na Harns (1995) ambao walichanganua maswala ya kialfabeti na ukuaji wake kihistoria.

Maswala ya grafolojia katika isimumitindo ni muhimu sana kwa kuwa yanatuwezesha kufasiri na kufafanua namna maswala hayo yanavyoathiri maana mbalimbali katika matini na namna grafolojia inavyozua athari za kiusanii katika tungo husika. Grafolojia inahusisha maswala yote yanayohusiana na othografia, uakifishaji na maswala yote yanayochangia kuonyesha namna lugha inavyotumia malighafi ya kigrafiki kwa lengo la kubeba ruwaza za kisarufi au kileksika. Lennard (2005) na Levenston (1992), wanaeleza vigezo vya kiuchanganuzi vya grafolojia. Wamehusisha isimu ya lugha na mitindo mbalimbali kwa kuvipanga vigezo vya kigrafolojia katika muundo maalum. Levenston anachanganua lugha ya kigrafolojia katika viwango vinne vikuu ambavyo ni maendelezo, uakifishaji, topografia na muundo wa kijumla wa kimaandishi.

Lennard (2005) alipinga mawazo ya Levenston. Alieleza maswala ya kimsingi katika uchanganuzi wa matini. Maswala haya ni kama vile maumbo halisi ya matini, sifa za kisintaksia miongoni mwa mengine. Kulingana naye, maswala ya uakifishaji hayahusu alama kavu za uakifishaji bali pia maswala ya kimaendelezo, mipakamaneno, maumbo mbalimbali ya herufi, utengano wa neno kwa neno, alama za uakifishaji, maneno tofauti kulingana na kimo cha herufi, uso wa herufi, rangi ya herufi na mahali ilipo herufi hiyo. Maswala haya ya kigrafolojia yatajitokeza katika uchanganuzi wa jumbe cheshi kiisimu. Kunazo jumbe cheshi zenye maandishi yenye maendelezo yasiyo sahihi kama mtindo wa kutoa ujumbe na maana miongoni mwa sifa nyingine kama hizi kama zitakavyojadiliwa katika sura zifuatavyo.

### 1.6.6 Ukiushi wa Kisemantiki

Kiwango hiki huhusisha maana katika lugha ya binadamu. Maana za maneno hufasiriwa kulingana na matumizi yake katika tamko la lugha. Maana zingine huwa si wazi humbidi mfasiri kuwazia kwa kina ili kuufasiri ujumbe husika. Leech, aeleza kuwa ukiushi wa kisemantiki ina maana ya maana zisizo wazi na ambazo hazina umantiki au huwa zina sifa ya uparadoksi. Ukiushi huu hudhihirisha kuwa neno laweza kuwa na maana isiyo ya kawaida au isiyozoeleka. Maana hutegemea matumizi yake haitegemei namna neno linavyojitokeza kwa

kulitazama tu kijuujuu. Katika jumbe cheshi za mtandao, ukiushi wa kisemantiki hujitokeza kimakusudi. Matumizi ya lugha ishara au ya kiistiari hujitokeza katika jumbe cheshi.Matumizi ya lugha yenye kinaya kwa mfano husababisha ukiushi wa kisemantiki kwa sababu maana ya juu au inayotamkwa siyo inayomaanishwa. Ukiushi wa kisemantiki katika jumbe cheshi utajadiliwa kwa namna mbili ambazo ni uhamishaji wa maana na uwongo wa kiusanii. Kila mojawapo wa vigezo hivi vitajadiliwa kwa kina katika sura zijazo.

### 1.6.7 Ukiushi wa Kileksika

Ukiushi huu unahusiana na uundaji wa maneno mapya. Katika jumbe cheshi, kuna maneno mapya yanayojitokeza katika jumbe maandishi za jumbe cheshi ambayo yanaonekana kukiuka sarufi sanifu ya lugha ya Kiswahili. Maneno mengine yameundwa ili kuzua ucheshi ambao ni sifa kuu ya jumbe cheshi za mitandao. Ukiushi wa kileksika pia hujitokeza wakati neno linapopata matumizi mapya kando na yale yaliyozoeleka kwa kawaida. mfano “kanyaga” linakuwa “kanyagia” kwa maana “kukataa na jambo” Katika sura ijayo tutajadili njia mbalimbali ambazo hii misamiati mipya huundwa namna inavyojitokeza katika jumbe cheshi. Njia hizi ni kwa mfano matumizi ya maneno misimu, kufaragua matumizi ya neno miongoni mwa njia nyinginezo.

### 1.6.8 Ukiushi wa Kisajili

Kigezo kikuu katika ukiushi wa kisajili ni kuchanganya sajili tofauti katika matini moja husika. Jambo hili hufanyika ili kuafikia ucheshi wa kiisimu ambayo ni sifa kuu ya kimtindo inayohusishwa na jumbe cheshi za kidijitali, kwa mfano sajili ya kidini inaweza kutumiwa katika muktadha wa sajili ya mazungumzo ya kawaida. Ukiushi wa kisajili utajadiliwa kama unavyojitokeza katika jumbe cheshi za kidijitali.


## 1.7 Nadharia za Uhakiki

Utafiti huu utaongozwa na nadharia mbili; nadharia ya semiotiki na nadharia ya elimumitindo. Nadharia hizi mbili zitachangiana na kuingiliana. Hii ni kwa sababu, jumbe cheshi za mitandao huhusisha ishara zinazofafanuliwa na nadharia ya Semiotiki. Aidha, jumbe tunazoshughulikia zinahusisha picha zinazoambatana na maneno. Tutaelekezwa na nadharia ya elimumitindo kuzihakiki picha pamoja na maandishi yanayojitokeza katika jumbe hizi. Vilevile, nadharia ya elimumitindo itatuelekeza kufafanua maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika jumbe cheshi.

### 1.7.1 Nadharia ya Semiotiki

Semiotiki ni elimu ya ishara. Ishara hizi zinaweza kuwa katika kundi au mojamoja. Elimu hii inahusu vile ujumbe unavyofafanuliwa na mpokezi. Haya ni kulingana na Aronoff na Rees-Miller (2008). Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Ferdinard De Sassure (1857-1913) kisha ikaendelezwa na Peirce (1991). Mwelekeo mkubwa wa nadharia hii ni kupendelea neno „matini" unawafanya baadhi ya wahakiki kuiita nadharia ya umatini. Nadharia yenyewe huchanganua jinsi kazi husika zinavyowasiliana na wasomaji. Nadharia hii haisisitizi tu maswala ya kifasiri au jinsi tunavyoifasiri kazi fulani tu bali pia usomaji wetu wa kazi fulani huwa na maana zilizo nazo kwa wasomaji wake.

Utafiti wa kisemiotiki hunuia kuchunguza uhusiano baina ya X = Y. X ni kitu kilichopo. Kinaweza kuwa neno, picha, kipindi katika runinga ama kitu kilichobuniwa na binadamu. Y ni maana inayotokana na kitu hicho. Kuchunguza maana ya Y ndio Semiotiki. Mchakato wa kuchunguza maana ya Y huitwa ufasiri. Mchakato wa kurekodi mawazo, ujuzi, au ujumbe unaitwa uwakilishaji katika nadharia ya Semiotiki (Danesi, 2003). Pierce anahusishwa na kielelezo cha ishara kinachohusishwa na pembe tatu.




**Mchoro 3: Uhusiano wa Ishara Kulingana na Pierce (1991)**

Kulingana na Pierce, kila ishara huwa yambwa au kitendwa kinachorejelewa. Kifasiri ni kile kinachochochewa katika akili ya anayeifasiri ishara hiyo. Kinachochochewa kinaweza kutazamwa kama ishara ya pili. Katika umbo hilo, kuna uhusiano baina ya ishara na jambo linalowasilishwa na mfasiri anayeipa ishara maana. Mfasiri huweza kuwa anayeufafanua ujumbe huo. Nadharia hii itatusaidia kufafanua namna jumbe za mitandao zinavyowasiliana. Kwamba, jumbe hizo au/pamoja na picha huwa ishara za kipekee za kisemiotiki ambazo huweza kutolewa fasiri fulani za kiisimujamii na mpokea ujumbe. Kwa mfano, jumbe za mitandao hutumiwa kueleza maoni na hisia tofauti za watu katika jamii husika.

Dhana moja muhimu inayohusishwa na Barthes (1981) ni msimbo. Anasema kwamba matini ya kifasihi inafaa kuvunjwa kwenye sehemu ndogo ndogo alizoziita leksia. Kulingana naye,

kila leksia hudhihirisha misimbo au kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri. Alizitambua aina tano kuu za misimbo ambazo ni nguzo muhimu katika nadharia hii.

Msimbo wa matukio unahusu namna matukio yanayopatikana katika matini fulani yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana kiusababishi. Kuna msimbo wa kihemetiki ambao unahusu taharuki. Msimbo huu hufumbatwa kwenye anwani ya matini fulani. Kwa kutazama jumbe za picha, tunajiuliza ni kwa nini ule ujumbe wa picha umejitokeza kwa namna fulani. Msimbo wa kiseme huhusisha seme ambazo ni elementi sababishi za kisemantiki. Ni elementi zinazotuwezesha kupata picha fulani. Ni namna mpokea picha atakavyoishia kuipata picha ya mhusika/wahusika wanaojitokeza kwenye ule ujumbe.

Msimbo wa kiishara unahusishwa na jinsi mpokea ujumbe anavyozivumbua maana za kiishara katika matini fulani. Kutokana na jumbe mbalimbali za mitandao ya kijamii wapokea ujumbe tofauti wanaweza kuvumbua maana ya picha fulani kwa namna moja au kwa namna tofauti. Pia kuna msimbo wa kirejelezi unaojengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelewa katika matini inayohusika. Urejelezi huu huunda uhalisia mahsusi kwa matumizi ya ishara zinazoeleweka na wapokea jumbe na hivyo kuipa kazi hiyo nguzo za kiutamaduni.

Tunaweza kusema kwamba jumbe zinazorejelewa katika utafiti wetu huenda zisieleweke na wapokezi walio nchi za mbali. Picha hizi kwa kiwango kikubwa zitang'amuliwa na Wakenya kwani zina vielekezi vya utamaduni wao. Tutazitumia nguzo nne kama mihimili ya kiuchanganuzi katika kuzihakiki jumbe cheshi za mitandao. Msimbo wa matukio utatuelekeza kufafanua jumbe zinazosheheni maswala ibuka mbalimbali yanayosababishwa na matukio ambayo huwa yamejitokeza hapo awali kiwakati. Msimbo wa kihemetiki unatuelekeza kuelewa mivuto ya kipekee inayojtokeza kwa kutazama jumbe hizi. Upungufu wa nadharia hii ni kuwa inachukulia kwamba ishara zote kila mahali na wakati wote zina maana. Inapuuza hali ambapo ishara zingine huwa hazijabeba ujumbe wowote, (Griffen, 1997: 118). Ni kweli kuwa Semiotiki ina hatari ya kuweka maana juu ya kila kitu kiasi cha kupoteza uhalisia. Hata hivyo, nadharia hii bado ina mashiko na binadamu ana wajibu wa kumakinika kuelewa mazingira, utamaduni na lugha yake.

### 1.7.2 Nadharia ya Elimu Mitindo

Nadharia hii ya isimumitindo iliasisiwa na mwanaisimu katika Geneva kwa jina Charles Bally (1916). Alisisitiza umuhimu wa lugha katika kujieleza na uamilifu wa lugha katika utangamano. Alieleza kuwa lugha huwasilisha hisia na fikira na kwa hivyo swala lolote la isimu ni lazima lihusishe lugha na fikira. Kwamba msemaji au mwandishi huipa fikira yake kuu sifa za kiisimu na kuihusisha fikira hiyo na uhalisia wa maisha. Kulingana na Bally, kuna swala la uchaguzi ambalo ndilo kigezo kikuu. Kwamba athari na sifa za kujieleza huafikiwa kwa uchaguzi huru kwenye mahusiano ya kileksika na pia mahusiano ya kisintaksia. Athari za kileksika na za kisintaksia huhusiana katika kueleza fikira mbalimbali hata ingawa kila mojawapo wa mahusiano hayo yana athari tofauti tofauti yanapojieleza. Jambo muhimu kutambua ni kuwa Bally haelezi jinsi njia tofauti za mawasiliano zinavyohusiana na yale yanayowasilishwa pamoja na maana mbalimbali zinazojitokeza.

Nadharia hii ina mihimili minne mikuu: Kwamba muundo wa lugha unahusiana na matakwa yaliyowekewa lugha hiyo inapotumiwa; Kwamba fikira huwa na vigezo viwili vikuu: Udhana na Usodhana. Udhana hutokana na imani za kijamii. Usodhana unaelezea tajriba ya mtu pamoja na hisia zake mbalimbali. Isimu hulenga chanzo cha udhana katika uamilifu wa lugha. Isimumitindo, kwa hivyo, inatumia uamilifu wa lugha kama kigezo chake kikuu. Isimumitindo hulenga kueleza namna lugha inavyojizoesha kuwezesha mawasiliano ya mawazo yoyote ya fikira za mwanadamu. Kwamba muundo wowote wa kueleza mtindo hutambua na kufafanua chanzo cha mawasiliano yasodhana kwa kutathmini uhusiano uliopo kwenye vipashio lugha na uwezo wa vipashio hivyo kuwasilisha mawazo yote yasodhana.

Spitzer (1967) mwasisi wa elimumitindo ya kisasa aliasisi mwelekeo tofauti wa mitindo. Alihusisha uzoefu na uamuzi alionao mwandishi. Mwelekeo huu unaeleza uhusiano baina ya mitindo ya uandishi na msukumo wa mwandishi. Kwamba kwa kuhakiki sifa za kimtindo, mhakiki atauona na kuuelewa mwonoulimwengu wa mwandishi. Riffatere (1959) anaona elimumitindo kama kigezo kinachoandaliwa akilini mwa msomaji na wala sio kigezo kinachowasilishwa na miundo ya kiisimu. Riffatere alipinga mwelekeo wa kutegemea mielekeo ya kiisimu katika kuhakiki kazi za uandishi. Maoni yetu ni kuwa uchanganuzi wowote wa kimtindo unafaa kuangazia matini yenyewe na pia kutathmini tendo lote kwa jumla la mawasiliano. Hapa maoni yetu ni kwamba msomaji ni kiungo muhimu sana katika swala nzima la uchanganuzi. Maoni ya Riffatere ni hayo hayo kuwa ufasiri wa msomaji ni wa

kutiliwa maanani na kwamba uchanganuzi wa matini na mtindo wake hauwezi kutenganishwa na majibu ya msomaji.

Riffatere anasema kwamba elimumtindo huangazia mbinu za kimtindo zinazotekeleza jukumu la kumzuia msomaji kuutabiri ujumbe muhimu. Utabiri kulingana naye husababisha usomaji wa juu juu. Kutotabiri hulazimisha umakinifu hivi kwamba kiwango cha mapokezi huwiana na kiwango cha ujumbe wenyewe. Halliday (1978:89) anasema kuwa lugha ina umuhimu mkubwa kama kiamuzi na kinachoamuliwa. Kwamba lugha hudhibitiwa na muundo wa kijamii, nao muundo wa kijamii hushikiliwa na huwasilishwa na lugha. Halliday anapendekeza vidhibiti lugha vitatu katika uamilifu wake. Kuna uamilifu wa dhana (unaohusiana na maana ya yanayorejelewa au yaliyomo katika ulimwengu wa msemaji). Pia kuna uamilifu wa kiutubinafsi kwa maana ya mitazamo na mielekeo baina ya msemaji au mwandishi na mpokezi au msomaji katika kubaini maana kimuktadha. Kidhibiti cha tatu kulingana na Halliday ni uamilifu wa kimatini. Mtazamo wa Halliday unaonekana kuegemea zaidi mpokezi badala ya matini yenyewe.

Stanley Fish (1980) aliupinga mtazamo wa Halliday kuhusu elimumitindo. Alieleza kuwa matini sio kiungo huru katika kufafanua maana bali ni athari za kimtindo ambazo hutokana na kuchanganua uamilifu wake kwenye akili ya msomaji. Kwamba maana ni matokeo ya tendo la kusoma matini fulani ili kuwezesha kuifasiri maana hiyo. Nadharia hii ya elimumitindo itatusaidia kufafanua jumbe cheshi za mitandao kwa kuchanganua fonimu, leksimu pamoja na maswala ya kisintaksia.

Vigezo hivi vyote huchangiana ili kuupa ujumbe maana. Aidha, nadharia hii itatusaidia kuchanganua jumbe hizi tukirejelea maswala mengine kama vile ya kisajili. Jumbe hizi zitaonekana kuegemea sajili tofautitofauti. Ni kupitia nadharia hii ndipo itawezekana kuyachanganua maswala ya kiisimu na matini kama kitengo kimoja. Hata ingawa vitengo hivi viwili ni tofauti, vinategemeana. Hii ina maana kuwa ni vigumu kwa mwanaisimu asiye na ujuzi wa kuhakiki matini au mhakiki asiye na maarifa ya kiisimu kuchanganua matini yoyote kiakademia kwa lengo la kuzalishia hukumu zenye urazini.

Nadharia hii ndiyo muhimu zaidi kwani itawezesha uchanganuzi wa jumbe za mitandao katika vitengo vya kiisimu ambavyo ni kigrafolojia, kimofolojia, kisintaksia, kileksika na pia kisemantiki. Maarifa ya kiisimu yatatusaidia kueleza matumizi ya lugha kwa kina kwa kuyahakiki huku tukiyalinganisha na matumizi ya kawaida ya lugha.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu utategemea data kutoka kwa mitandao. Data itachotwa kutoka kwa wavuti mbalimbali. Wavuti hizi humilikiwa na huendeshwa na wanaotayarisha jumbe cheshi hizi na huzisambaza kwa wawasilianaji mbalimbali kupitia mtandao. Yeyote anaweza kufungua wavuti hizi na kuzisakura jumbe cheshi zenyewe. Wavuti tunazonuia kuchota data yetu kwazo ni kama zifuatazo: Nairobiwire.com, Facebook.com, Mpasho.co.ke, Trendkenyaonlineblogs, Youthvillage.co.ke, Funnyton.com, Classic105.com, Hivisasa.com na Kenya crazymedias.com.

### 1.8.1 Sampuli Kielelezo

Sampuli kielelezo ni kundi la wajibu wanaoteuliwa ili kuwa kama kiwakilishi cha jamii pana. Tunanuia kuchota data yetu ambazo ni jumbe cheshi za mtandao kutoka kwa jumla ya wavuti kumi. Katika kusakura kwetu tuligundua kuwa kuna takribani wavuti 20 ambazo hujihusisha na jumbe cheshi za lugha ya Kiswahili. Walengwa ni lazima wawe na sifa moja kuu inayowafananisha. Tutatumia akisami ya nusu ya wavuti hizi ishirini ili idadi ya sampuli lengwa iwe takribani wavuti kumi. Tutatumia aina ya uteuzi wa sampuli wa mtabakisho ambayo huhusisha uteuzi wa idadi maalum ya jumbe cheshi kutoka kwa kila mojawapo wa wavuti hizo kumi ambazo ndizo sampuli kielelezo. Wavuti hizi kumi zina takribani jumbe cheshi 150 ambazo zinatumia lugha ya Kiswahili katika maandishi yazo. Miongoni mwa jumbe cheshi hizi 150, tutaweza kuchagua jumla ya jumbe cheshi 100 ambazo ndizo zitakazokuwa idadi ya walengwa tutakayotumia kuafikia sampuli kielelezo.

Tutatumia fomula ifuatayo kulingana na Yamane katika Minium (1978).

$$n = \frac{N}{1+N(e)^2}$$

n = idadi ya sampuli

N = walengwa

e= kiwango cha hitilafu (+ ama - 10%).

Jedwali lifuatalo limetayarishwa kutoka kwa fomula hii ya Yamane.Jedwali lina matokeo tofauti ya n kulingana na idadi tofauti ya N. Jedwali linaonyesha idadi tofauti ya walengwa ambapo kulingana na utafiti wetu ni takribani 100. Pia, jedwali linaonyesha viwango tofauti vya hitilafu (+ au -5%,7%,10%). Tunanuia kutumia kiwango cha hitilafu cha + au-10%

katika utafiti wetu. Kwa hivyo, idadi ya jumbe cheshi tutakazotumia kama sampuli kielelezo zitakuwa jumla ya jumbe cheshi 51.

Jedwali 1. Jedwali la fomula ya sampuli kielelezo kulingana na yamane (1967)

| **Idadi ya Walengwa** | **Idadi ya Sampuli na Viwango vya Hitilafu** | | |
|---|---|---|---|
| | + AU – 5% | + AU -7% | + AU – 10% |
| 100 | 81 | 67 | 51 |
| 125 | 96 | 78 | 56 |
| 150 | 110 | 86 | 61 |
| 175 | 122 | 94 | 64 |

### 1.8.2 Mbinu za Ukusanyaji Data

Utafiti huu kama tulivyotaja hapo awali unategemea data kutoka mtandao. Utazamaji wa moja kwa moja wa jumbe cheshi hizi zikiwa kwenye mtandao utafanyika kisha tutazisakura kutoka kwa wavuti zilizotajwa kisha zitahifadhiwa kwa msaada wa tarakilishi. Uchanganuzi wa kina kuhusu namna ukiushi wa kiisimu unavyojitokeza kwenye jumbe cheshi hizi utafanyiwa katika maktaba. Tunalenga kuzisakura jumbe cheshi ambazo zina sifa ya kutokuwa na utubinafsi, pia jumbe cheshi sampuli hazitatarajiwi kuonyesha maswala yoyote ya ngono na aidha zisiwe na miegemeo mikali ya kisiasa bila kusahau uzingativu wa tafsida katika lugha na maana zake.

Baada ya kupata jumbe cheshi takribani hamsini na moja, zitaweza kupangwa kutegemea ukiushi wa kiisimu unaowasilishwa na jumbe cheshi husika. Kila jumbe cheshi itapewa nambari yake. Jumbe cheshi mbili au tatu zinazowasilisha ukiushi sawa zitapewa nambari sawia. Kutakuwa na uwezekano wa jumbe cheshi fulani kurudiwa katika kufafanua maswala tofauti ya ukiushi. Ni muhimu kutaja kuwa jumbe cheshi inahusisha fremu na pia jumbemaandishi. Uchanganuzi wetu utaegemea zaidi jumbemaandishi kwa sababu ya

kujibana kwenye upeo na mipaka ya utafiti wetu. Uchanganuzi wetu wa jumbe cheshi kiisimu utafanyiwa katika maktaba.

# SURA YA PILI

# NADHARIA YA JUMBE CHESHI

## 2.0 Utangulizi

Jumbe cheshi ni kigezo cha utamaduni au mfumo wa kimtindo unaopitishwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa njia ya kuiga au kwa njia nyingine yoyote ile; jumbe cheshi ni mwigo fulani, video au maandishi fulani ambayo kwa kawaida huzua ucheshi ambao unaigwa kwa kunakilishwa na kisha husambazwa upesiupesi na watumizi mtandao huku ikifanyiwa mabadiliko machache wakati mwingine. Maelezo haya yanaeleza dhana moja kwa namna mbili tofauti. Haieleweki ni vipi dhana ya kitamaduni itakavyovuma kwa muda mchache katika mtandao halafu kufifia baada ya muda fulani. Ufafanuzi ufuatao wa kinadharia unalenga kueleza aina tofauti za jumbe cheshi kwa kuzingatia vigezo tofauti.

Kuna jumbe cheshi za kijadi na jumbe cheshi za kidijitali. Haya ni kulingana na Blackmore (2001) anayeeleza kwamba tunapoiga mtu mwingine kuna kigezo kinachopokezanwa; kigezo hiki kinaweza kupitishwa na kupitishwa hivi kwamba kinapenyeza miongoni mwa watu kwa njia hii. Kigezo hiki kulingana na Blackmore chaweza kuwa dhana, fikira, maagizo fulani, tabia au taarifa fulani. Vigezo hivi ndivyo anavyovirejelea kama jumbe cheshi. Kwa ufafanuzi huu, tunaweza kutambua ulimwengu tunaoishi, ubinadamu wetu, hisia zetu kwa jumla kama aina ya jumbe cheshi. Blackmore anayahusisha maelezo yake na mwanabayolojia Dawkins (1976) aliyeasisi neno “meme” ili lieleweke kwa namna linavyoeleweka kwa sasa. Dawkins aliirejelea hata dini kama jumbe cheshi. Kulingana naye, jumbe cheshi nzuri ni lazima iwe ya kutegemewa, pia iwe ya kudumu na iweze kunakilishwa na kuigwa mara nyingi iwezekanavyo huku ikifanyiwa mabadiliko machache.

Dawkins alihusisha mchakato mzima wa namna uzazi unavyorithisha tabia na sifa mbalimbali za mtu na mchakato wa namna jumbe cheshi zinavyosambazwa kutoka kwa kiini chake hadi kwa ubongo mmoja hadi mwingine kupitia uigaji. Dawkins (1976) aliziona jumbe cheshi kama viumbe hai namna tu chembechembe za kurithisha kizazi zinavyokuwa hai. Mawazo ya Dawkins yanaungwa mkono na Humphrey (1976) anayesema kuwa jumbe cheshi zinastahili kuchukuliwa kama viungo vyenye uhai. Humphrey anasema,

„Unapopanda jumbe cheshi zalishi katika ubongo wangu, kwa njia fulani inakuwa kama kimelea katika ubongo wangu na unageuza ubongo wangu kuwa chombo cha kuikuza

hiyo jumbe cheshi kwa namna sawa na namna kirusi kinavyokuwa kimelea katika mwili wa kiumbe.‟

Hii ina maana kwamba ni lazima inakilishwe na kuigwa mara nyingi iwezekanavyo na pia idumu muda mrefu iwezekanavyo. Tukizichanganua jumbe cheshi kutoka kwa mwelekeo huu, tunaweza kusema kuwa hata wimbo fulani, hatua za kucheza densi au fikra yoyote ile vyote ni jumbe cheshi. Mawazo ya kuhusisha jumbe cheshi na utamaduni yanaeleweka katika mwelekeo huo. Dawkins alilinganisha jumbe cheshi na chembechembe za kizazi kama kiungo cha kupitisha sifa fulani za kibinadamu. Alieleza jumbe cheshi kama zinazopitisha maswala ya kitamaduni kama vile lugha, desturi, mitindo ya mavazi na ile ya ulaji. Neno "jumbe cheshi" latokana na neno la Kigiriki „mimene‟ kwa maana „kilichoigwa.‟ Jumbe cheshi huchipuka kutokana na swala nzima la kuiga utamaduni wa jamiihusika.

### 2.1 Jumbe Cheshi za Kidijitali

Shifman (2013) anadai katika utafiti wake kuwa jumbe cheshi zilivumbuliwa miaka mingi iliyopita hata kabla ya enzi ya kidijitali. Anasema kuwa mfumo wa mtandao ndio uliowezesha jumbe cheshi hizi kuwa vigezo vinavyoonekana kila siku. Miongoni mwa watumizi mtandao, ni mtindo wa kawaida kuziunda jumbe cheshi na pia kuzisambaza kwa watumizi mtandao wengine. Jumbe cheshi za kidijitali husambazwa na watumizi mtandao kama njia ya kueleza dhana au fikra kwa njia ya kimaandishi au picha. Tofauti kuu baina ya jumbe cheshi za kidijitali na za kijadi ni kuwa, jumbe cheshi za kidijitali sio lazima idumu kiwakati. Kwa upande mwingine, jumbe cheshi za kijadi huwa dhahania kwa kiasi fulani lakini jumbe cheshi za kidijitali hufafanuliwa kwa matamko halisi kupitia wavuti mbalimbali.

Shifman alichanganua pia viwango mahsusi ambavyo jumbe cheshi za kidijitali husambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, namna zinavyobadilishwa, na aina ya jumbe cheshi ambazo huwa na sifa ya kudumu. Katika ufafanuzi wake, alitambua wavuti kama vile Youtube, Facebook au Twitter zinavyochangia kwa kiasi kikubwa kuzipa jumbe cheshi mandhari mazuri ya kutengenea zinapoundwa na kusambazwa. Hii ni kwa sababu, jumbe cheshi moja huweza kufikia maelfu kwa maelfu ya watu katika kipindi kifupi mno. Kwamba kinyume na mawasiliano ya ana kwa ana ambapo anayewasiliana anaweza kugeuza ujumbe kutoka hali asilia kulingana na utubinafsi wake, katika mfumo wa kidijitali, mawazo yanaweza kusambazwa bila mageuzi yoyote kufanyika.

Aidha, kuna wavuti zingine zinazowapa watumizi wake fursa ya kujiundia jumbe cheshi zao au kuzifaragua zilizopo. Jumbe cheshi tunazochanganua kama data yetu ya kiuchunguzi ni zile za kidijitali ambazo zina vigezo vya picha na/au maandishi na ambazo zimetengenezwa kwa ujuzi wa kiteknolojia ili kudhihirisha maana fulani. Kwa ujumla, jumbe cheshi hizi hueleza fikra na maoni kwa hekima na kwa mitindo mbalimbali ya lugha illiyokiushwa na pia kwa namna ya kukejeli hali tofautitofauti. Aidha, huwa zina mwelekeo wa kuhukumu uzuri au uhafifu wa hali tofautitofauti.

## 2.2 Muundo wa Jumbe Cheshi

Kama dhana ya kisasa, jumbe cheshi zimetambuliwa kupitia njia ya mtandao. Jumbe cheshi hazitumiwi kuzua ucheshi tu bali pia huwasilisha jumbe tofautitofauti. Huzua ucheshi na pia kukejeli watu na hali mbalimbali wakati huohuo. Katika kuziweka jumbe cheshi kwenye kategoria zake, taaluma ya isimutambuzi inachukuliwa kuwa msingi wa kulipa neno maana. Isimutambuzi husaidia katika kufafanua maana za jumbe cheshi. Kulingana na Kovecsces (2015), mwelekeo wa isimutambuzi una msingi wake katika kufafanua maana mbalimbali.

Kwanza, kuna jumbe cheshi aina ya proto. Jumbe cheshi aina hizi hujumuisha maandishi ambayo huweko sehemu ya juu ya picha na pia sehemu ya chini ya picha. Ufafanuzi wa jumbe cheshi aina hizi sio wa aina ya kimlalo bali kinachoonekana kwanza ni picha halafu maana zinazobebwa na maandishi hung‟amuliwa baadaye pamoja na mitindo yake ya kiisimu. Huu hapa ni mfano mwafaka wa jumbe cheshi aina ya proto.



**Picha 1: Muundo wa Jumbe Cheshi**

Kuna jumbe cheshi ambazo ni aina tofauti ya jumbe proto ambazo huwa na maandishi sehemu ya chini pekee. Mfano wa jumbe cheshi aina hii upo hapa chini.




**Picha 2: Muundo wa Jumbe Cheshi na Maandishi Sehemu ya Chini**

Pia kuna kuna jumbe cheshi ambazo hazina picha yoyote lakini tunazitambua kuwa jumbe cheshi kulingana na mtindo wa upigaji chapa kwenye maandishi yake. Mfano ni kama ufuatao hapa chini;




**Picha 3: Muundo wa Jumbe Cheshi bila Picha**

Kuna zingine ambapo maandishi hayawekwi sehemu ya chini ama juu bali huwekwa sehemu fulani pale katikati mwa picha. mfano ufuatao wa jumbe cheshi utaeleza aina hizo za jumbe cheshi;





**Picha 4: Muundo wa Jumbe Cheshi na Maandishi katikati mwa Picha**

Kuna jumbe cheshi zingine ambazo huundwa kwa ishara za picha pekee. Mfano ni kama ufuatao hapa chini.




**Picha 5: Muundo wa Jumbe Cheshi na Picha pekee**

Kovesces (2006**)** anadai kuwa jumbe cheshi aina ya proto ni mfano mzuri wa jumbe cheshi katika kategoria ya dhana. Kategoria ya dhana ina maana kuwa dhana fulani zinazohusiana na maisha ya binadamu huwasilishwa kupitia aina hizi za jumbe cheshi proto. Mfano wa dhana hizi ni maswala ya kimapenzi, ya kijamii. Vilevile, dhana za kiisimu kama vile mpangilio wa sauti au maneno hudhihirika katika aina ya jumbe cheshi za kiproto. Jumbe cheshi proto kwa mawazo haya itachanganuliwa kama jumbe cheshi iliyoundwa kwa picha na jumbe maandishi. Kuna baadhi ya jumbe cheshi ambazo huundwa kwa picha pekee au maandishi pekee kama tulivyosema hapo juu.

## 2.3 Fremu ya Jumbe Cheshi

Kovesces (2006**)** anaeleza kwamba iwapo jumbe cheshi ni maumbo yaliyoundwa kwa madhumuni fulani, basi ni lazima pawepo na maana muhimu sana inayobebwa na umbo hilo lote. Maana hiyo sio lazima ionekane wazi kwenye umbojumbe cheshi hilo. Kwamba katikati ya picha na maandishi hayo ya kidijitali, mfasiri hung‟amua fikra, maoni, mawazo, mgeuko wa kiutendaji, tashtiti n.k Uamilifu wa kimawasiliano na maana yenyewe ya jumbe cheshi huvumbuliwa kama maana zinavyovumbuliwa katika matini nyingine yoyote ile.

Picha zinazotumika kama fremu katika wavuti ili kuunda jumbe cheshi huwa ni maumbo yanayotumiwa kuzalisha jumbe cheshi tofauti kwa mtindo wa uigaji. Maumboigwa haya huhimiza ubunifu zaidi kutokea katika kuunda jumbe cheshi nyingi zenye mawazo tofauti. Katika kutekeleza haya, fremu moja ndio hutumiwa kama umboigwa. Uchaguzi wa fremu hulingana na maana inayokusudiwa kutoka kwa jumbe cheshi husika. Wazo hili lina maana kwamba picha inayotumiwa kama fremu inaweza kuwa ya mtu maarufu katika jamii wahusika katika drama za video n.k. Jambo hili lina maana kwamba mfasiri huhitaji ufahamu wa kando kuhusiana na mhusika aliyetumiwa kama fremu kwenye jumbe cheshi. Maarifa kuhusiana na matendo ya mhusika huyo huchangia katika kufasiri maana ya jumbe cheshi husika. Hii hapa ni mifano ya jumbe cheshi zinazowatumia wahusika maarufu kama fremu ya jumbe cheshi hizo.





Baba Mtakatifu wa Kikatoliki

William Sosion- Katibu Mkuu wa Chama Cha walimu KNUT.

**Picha 6 (a) na (b): Jumbe Cheshi Zinazowatumia Wahusika Maarufu kama Fremu**

## 2.4 Jumbe Cheshi Tangazi

Hizi ni aina ya jumbe cheshi ambazo msukumo wa kuziunda hutokana na mada ibuka na maarufu kama vile siasa za nchi au michezo ya dunia miongoni mwa maswala ibuka mengine mengi. Katika dhana hii, jumbe cheshi hizi zinaweza kuwa jumbe cheshi proto au zisiwe za kiproto; italingana na maumbo yake. Aina hizi zaweza kuwa na maandishi sehemu ya juu na chini au hata zisiwe na maandishi yoyote. Tofauti kuu baina ya jumbe cheshi tangazi na zenye miundoigwa ni kwamba jumbe cheshi tangazi zinakuwa maarufu katika muda mchache tu. Hii ni kwa sababu zinaundwa kutokana na matukio maalum yanayochipuka kisha yanasahaulika. Jumbe cheshi tangazi hizi zitatekeleza wajibu wake katika kipindi hicho maalum wakati swala fulani limechipuka kisha kusambazwa kwake kunakoma wakati swala lingine ibuka linapochipuka. Hapa chini tumetoa mifano ya aina hizi za jumbe cheshi tangazi.







**Picha 7 (a) na (b): Jumbe cheshi Tangazi**

## 2.5 Dhana Mfanano

Kovecses anafafanua dhana mfanano kama namna ishara ya neno, kirai au miondoko katika lugha ishara hufanana na dhana inayowakilishwa. Kwamba kuna hali ya uasomofu baina ya miundo ya kidhana na miundo ya kiisimu. Dhana mfanano ni kama mafumbo yanayowakilisha dhana fulani. Kovecses (2006) anaeleza kwamba uhusiano wa karibu uliopo baina ya elementi maandishi na elementi picha husababisha mbano wa kimaelezo. Jumbe cheshi zinazotokana na maumboigwa huwa na mbano wa kiwango cha juu kwa sababu ya mfanano kwenye sehemu moja ya jumbe cheshi husika. Kuna hali ambapo tukiondoa picha ili kuachwa na maandishi pekee, jumbe cheshi yenyewe haitoi maana yoyote yenye urazini.

Kwa hivyo, tuna maana kuwa katika jumbe cheshi aina ya proto, maandishi na picha hukamilishana ili kuzua maana iliyokusudiwa.

## 2.6 Ucheshi katika Jumbe Cheshi

Sifa kuu inayoonekana kuhusishwa na jumbe cheshi za mtandao ni namna zinavyozua ucheshi mwingi hata katika kueleza maswala nyeti. Ucheshi wa jumbe cheshi hutokana na sababu mbalimbali bali na matumizi ya mbinu za kiuandishi. Kovecses (2006) anasema kwamba, jambo moja muhimu mfasiri analotambua kwenye matini kutoka kwa mtazamo wa kiisimutambuzi ni mbinu za kiuandishi katika maelezo yoyote yale. Mbinu hizi ni kama vile metonimu, mafumbo, na uhulutishaji. Anasisitiza zaidi kuwa mbinu hizi za kiuandishi hazitoshi wala si muhimu sana katika kusababisha ucheshi wa jumbe cheshi. Sababu ni kuwa, kuna matamko ya kicheshi ambayo hayana mbinu zozote za kiuandishi zilizotajwa. Pili, kunayo matamko ambayo yanahusisha mbinu za kiuandishi lakini hayazui ucheshi wowote. Kuna mambo mawili yanayoelezwa kuchangia katika ujenzi wa mawazo ya kicheshi. Katika upande mmoja, uelewa wa maana ya jumbe cheshi huhitaji ufahamu wa awali wa maarifa fulani. Kwa upande mwingine, mawazo yaliyosalia na yanayohitajika ni ufahamu wa dhana zisizokubaliana wala kushikamana kimantiki. Katika dhana za maarifa yanayohusika, dhana hizi za kimaarifa zinaweza kuwa mbinu za uandishi au dhana halisi.

Kovecses (2015) alitambua dhana zifuatazo zisizokubaliana; Hali halisi na iliyowazwa; Yanayowezekana na yasiyowezekana; Yanayokubalika kijamii na yasiyokubalika (miiko); Idadi kubwa au nyingi na idadi ndogo au chache; Mambo asilia na yaliyozuliwa; Tathmini chanya na hasi; Kitendo na tukio; Mantiki zisizokubaliana; na Maswala yasiyokubaliana kiisimu na kidiskosi.

Ushahidi wa ucheshi wa kiisimu unadhihirika katika kila mojawapo wa dhana hizo zisizokubaliana. Jumbe cheshi hudhihirisha utata wa kiwango cha juu kuliko matamko ya kiisimu na kwa hivyo dhana zilizoorodheshwa hapo juu zinaweza kujitokeza mtawalia katika jumbe cheshi moja husika. Kwa mfano tukirejelea jumbe cheshi ifuatayo.





**Picha 8: Jumbe Cheshi ya Ucheshi**

Kwa kurejelea athari za kiucheshi katika jumbe cheshi iliyo hapo juu, mambo yafuatayo yasiyokubaliana yanajitokeza. Hali halisi na iliyowazwa, yanayowezekana na yasiyowezekana, mambo asilia na yaliyoundwa, mantiki zisizokubaliana, maswala ya kiisimu na ya kidiskosi yasiyokubaliana.

Katika kuhitimisha tunaweza kusema kuwa jumbe cheshi haziwezi kuwekwa katika kategoria moja pekee kwa mfano ya jumbe cheshi proto pekee. Hii ni kwa sababu kuna vigezo vingine vya ziada ambavyo ni muhimu sana kuvitambua ili kufafanua muundo wa jumbe cheshi kijumla. Vigezo hivi ni kama vile umbo, muda wa kudumu kwa jumbe cheshi ambao hutegemea mada inayohusika, pia kuna idadi za mbinu za kiuandishi zinazohusika. Kwa mfano, jumbe cheshi tangazi hutumia mbinu nyingi za kiuandishi kuliko zile za maumboigwa. Jambo lingine muhimu kulitambua ni kuwa ingawa jumbe cheshi tangazi huundwa kwa ufahamu kuwa hazitadumu sana kiwakati, huwa zinang‟ang‟ania katika usambazaji wake wa idadi nyingi iwezekanavyo wa jumbe cheshi aina hizi.


Tunaporejelea jumbe cheshi za maumboigwa, tunachukulia kwamba sio jumbe cheshi fulani mahsusi yenye sifa fulani mahsusi ambayo ina uwezekano wa kudumu zaidi lakini cha kutiliwa maanani zaidi ni hilo umboigwa au fremu ambayo hubeba maana yenyewe. Tunaporejelea dhana ya ucheshi, kila jumbe cheshi inategemea dhana fulani zisizokubaliana wala kushikamana. Hili ndilo jambo la kimsingi katika mchakato mzima wa uundaji jumbe cheshi. Hii ni kwa sababu, ili kuunda jumbe cheshi, ni lazima pahusishwe vigezo viwili vinavyoletwa pamoja hata ingawa vigezo hivyo vinadhaniwa kuwa tofauti katika uasilia wake. Tutatumia michoro maumbo yafuatayo kuelezea miundo na kategoria za jumbe cheshi.

**2.7** Muundo kwa kurejelea dhana za Urasmi





Kwa mujibu wa Kovecses (2015)

## 2.8 Muundo kwa kurejelea Muda wa Kudumu




Kwa mujibu wa Kovecses Zoltan, (2006)

**2.9 Muundo kwa kurejelea Kiasi cha Mbinu za Kiuandishi kilichotumiwa pamoja na Ukiushi**




Muundo wa jumbe cheshi kwa mujibu wa Kovecses (2006)

**2.10 Utata wa Memetiki**

Katika jarida Shifman (2013), maoni mojawapo kuhusu jumbe cheshi yanayojitokeza ni kuwa jumbe cheshi ni chombo kinachoudhi. Kwamba, tangu Dawkins kuhusisha jumbe cheshi na chembechembe za kizazi zinazosambaza utamaduni kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, jumbe cheshi kimekuwa kigezo kikuu cha mjadala hasa na wasomi. Wengine wanaonekana kuzipuuzilia mbali kabisa. Wanaoziunga mkono husisitiza kuwa jumbe cheshi zinaweza kutumiwa kufafanua maswala yoyote yale ya mwanadamu. Kwa upande mwingine, wanaozipuuza hushikilia kwamba jumbe cheshi haziwezi kutegemewa kuleta mabadiliko yoyote katika jamii na wanaziona kama "vitu bure!" Wataalamu mbalimbali kama vile Knobel na Lankshear (2007), Bernett (2003), Burgess (2008), walitumia jumbe cheshi kama kigezo kikuu katika kuelezea maswala fulani ya kiutamaduni. Maoni yetu ni kuwa tunafaa kuzichunguza jumbe cheshi kama kifaa cha kimawasiliano.

Memetiki ni kitengo cha kinadharia kinachohusika na kufanya majaribio ya kisayansi kuhusu jumbe cheshi. Hujihusisha na ufafanuzi, uzalishaji, usambazaji na ukuaji wa jumbe cheshi katika jamii. Wataalamu wengine wamekuwa wakipinga memetiki kwa madai manne makuu. Swala la kwanza ni kuhusu udhahania wa jumbe cheshi. Wanashikilia kwamba hakuna makubaliano kuhusu maana halisi ya jumbe cheshi. Wanauliza swali "Jumbe cheshi ni nini hasa?" Pili ni hali ya utamaduni unaotumiwa kama kiini kikuu cha jumbe cheshi. kuna tetesi kuwa una ufinyu na msukumo wake mkuu ni tamaa ya fedha. Kwa sababu hii hauwezi kutegemewa ili kufafanua tabia na maswala tata ya binadamu. Tatu, ni ule uteuzi wa kimakusudi na utovu wa udhabiti wa jumbe cheshi. Jambo hili limezua mjadala mkali kuhusu namna ya kudhibiti jumbe cheshi. Mwisho ni kuwa wanaozipinga jumbe cheshi hushikilia maoni kuwa hazina umuhimu wowote katika jamii na wala hazitoi mchango wowote zaidi ya yale yanayofafanuliwa na kitengo cha isimu pamoja anthropolojia ya kitamaduni.

Kwa upande mwingine, wanamemetiki hujishungulisha na maswala ya jumbe cheshi kwa sababu tatu kuu muhimu. Kwanza ni kwamba jumbe cheshi hueleweka kama ujumbe wa kiutamaduni unaopitishwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine ila kwa mwendo usio wa kasi huafikia viwango vya juu katika kupokezanwa. Hata ingawa zinasambazwa kwa viwango vidogovidogo, jumbe cheshi huishia kusababisha athari kubwa katika jamii kwa kuwa huathiri akili, tabia na matendo ya makundi jamii. Sababu ya pili ni kuhusu namna jumbe cheshi zinavyozalishana kwa kuigaigwa kisha zinasakurwa, kuundwa tena na kusambazwa tena na tena katika mtandao. Jambo la tatu na la mwisho la wanamemetiki kuzitetea jumbe cheshi ni namna zinavyoingia katika jamii kwa njia yenye ushindani na uteuzi maalum. Hii ni kwa sababu jumbe cheshi hutofautiana kiubora kwa namna zinavyojihusisha na utamaduni wa jamiihusika.

# SURA YA TATU

# UKIUSHI WA KISARUFI KATIKA JUMBE CHESHI

## 3.0 Utangulizi

Sheria za kisarufi katika lugha yoyote ile ni nyingi na kwa hivyo uwezekano wa hali ya ukiushi kutokea katika kiwango cha kisarufi ni wa kiwango cha juu vilevile. Katika kufafanua aina tofauti za ukiushi ni muhimu kuelewa mpaka uliopo baina ya kitengo cha kimofolojia (kitengo kinachohusiana na sarufi ya maneno) na kitengo cha kisintaksia ambacho ni kitengo kinachohusiana na sarufi ya mipangilio ya maneno hayo katika sentensi. Katika kuchanganua jumbe cheshi katika viwango hivi, tutaweza pia kuchanganua jumbe cheshi katika kiwango cha kileksika ambacho kinahusisha uundaji wa maneno mapya. Aidha tutachanganua ukiushi wa kiisimu wa jumbe cheshi katika kiwango cha kigrafolojia, cha kisemantiki na katika kiwango cha kisajili.

Kuna namna ambavyo picha, jumbemaandishi pamoja na maana zinavyohusiana ili kuzua jumbe za kijamii, kisiasa na hisia mbalimbali ama namna zinavyowatumbuiza wasomaji wake kwa njia yenye upekee. Uhusiano huo wa picha na jumbe pamoja na maana unaweza kufasiriwa kwa kuongozwa na nadharia ya semiotiki tunayoitumia kuchanganua swala letu la utafiti. Uchanganuzi wa kiisimu wa jumbe cheshi hizi utatuwezesha kuonyesha kuwa picha, maandishi na sanaa zinahusiana kwa pamoja kama njia mbadala ya kuwasiliana katika kuzua maana mbalimbali.

Wazungumzaji wa lugha yoyote ile wanatambua mifumo yote ya kisauti, maneno pamoja na miundo mbalimbali ya sentensi. Pia wanaelewa mipangilio ya maneno na mofimu katika sentensi za lugha yao. Katika kazi ya kisanii, mwandishi hutumia lugha inayokiuka sheria hizi za kisarufi. Lugha hii ndiyo inayorejelewa kama iliyochimuzwa kiisimu. Ni namna mwandishi anavyounda lugha ambayo imekiuka sheria zilizokubalika katika lugha yotote ile ya kawaida. Katika utafiti wetu kama tulivyosema hapo awali, tutarejelea swala la ukiushi katika viwango vitano vya kiisimu ambavyo ni mofolojia, sintaksia, kileksika, kigrafolojia na kiwango cha kisemantiki. Katika kuchanganua viwango hivi, tutachanganua dhana mbili za uchimuzi ambazo ni ukiushi na usambamba.

Ukiushi ni uteuzi wa kibinafsi wa kiisimu ambao humpa motisha au msukumo maalum mwandishi na pia kwa msomaji. Ukiushi unahusisha pia maana ya kazi na tathmini ya kisanii inayohusishwa na ufafanuzi wa maana. Ni kupitia swala la uchimuzi ndipo matini fulani

huhesabiwa kuwa yenye upekee wake. Tunaweza kuyarejelea maswala ya ukiushi katika sanaa kama sajili maalum ya kuitambulisha kazi husika. Kama tulivyosema hapo awali, uchimuzi unahusisha maswala mawili ambayo ni ukiushi na usambamba. Ukiushi katika sarufi utajitokeza kila wakati ambapo kaida za kisarufi zinapovurugwa kwa njia yoyote ile. Swala la ukiushi huwezekana katika viwango vya kisarufi au vya kisemantiki. Ukiushi ni hali ya kuondokea matarajio ya lugha katika viwango tofauti kama vile kiwango cha semantiki, kileksika, kisarufi au kifonolojia. Vilevile, ukiushi ni hali ya kuondokea matarajio katika kiwango cha kisarufi kwenye kitengo cha sentensi au virai.

Ukiushi unaweza kuwa wa kimuktadha pia ambapo mtumizi lugha anaweza kutumia lugha isiyoendana na muktadha wa mazungumzo. Kwa mfano, kutumia lugha isiyo rasmi katika muktadha rasmi. Ukiushi unaweza pia kujitokeza katika matumizi ya vigezo fulani vya lugha kwa mpangilio maalum. Mfano, urudiaji wa kirai mahsusi. Swala la usambamba linaingilia hapa kama kigezo mwambatano cha ukiushi. Ili kufafanua ukiushi mbalimbali wa kisarufi katika jumbe cheshi, ni jambo muhimu kutaja kuwa sarufi inahusisha maswala ya kimofolojia yanayohusisha miundo ya maneno na pia maswala ya kisintaksia yanayohusisha mpangilio wa maneno katika sentensi. Aidha, tutachanganua maswala ya kileksika yanayohusiana na uundaji wa msamiati katika lugha, maswala ya kigrafolojia yanayohusiana na ukiushi wa kaida za kimaandishi na ukiushi wa kisemantiki unaohusiana na maana za jumbe cheshi husika. Vilevile tutajadili ukiushi wa kisajili kama unavyojitokeza katika jumbe cheshi mbalimbali.

### 3.1 Dhana ya Ukawaida na Usanifu wa Lugha

Katika kueleza swala la ukiushi wa kisarufi katika jumbe cheshi, tutahusisha ufafanuzi wa ukiushi huu katika mielekeo miwili ya ukiushi. Kuna ukiushi ndani na ukiushi nje. Hii ina maana kuwa, tutachanganua maswala ya ukiushi wa kisarufi katika vitengo hivyo viwili ambavyo ni usanifu nje na usanifu ndani.

#### 3.1.1 Usanifu Nje

Tutachukulia kwamba maswala ya kawaida ni uwepo wa vigezo vyote vya muundo wa kiisimu ambavyo haviko katika jumbe cheshi tunazozichanganua. Hii ina maana kuwa ukiushi utachukuliwa kuwa vigezo vyote vya muundo wa kiisimu vinavyobainika wazi kwenye jumbe jumbe cheshi zinazochanganuliwa. Kwa mawazo haya, tutachukulia kuwa sarufi ya lugha ya Kiswahili ina miundo miwili. Kuna muundo wa vigezomsingi unaoshikilia kwamba sarufi ya Kiswahili ina kategoria zifuatazo pamoja na ishara zake: S-sentensi; RN-

kirai nomino; Kib-kibainishi; Rt-kirai kitenzi; T-kitenzi; N-nomino; V-kivumishi; E-kielezi; H-kihusishi; U-kiunganishi; I-kihisishi. Kila muundo wa sentensi huongozwa na sheria miundo virai mahsusi. Sarufi miundo virai hutumia kategoria za maneno yaliyoorodheshwa hapo juu. Pia kuna kigezo cha ugeuzaji kinachohusu sheria miundo virai tulivyotaja hapo juu.

### 3.1.2 Usanifu Ndani

Kila matini huwa na sheria au kawaida zake kulingana na lugha husika. Kwa mfano, katika kiwango cha kileksika, kuna aina tofauti ya msamiati unaotumiwa. Msamiati fulani usio rasmi hudhihirisha ukiushi iwapo utatumiwa katika mazingira ya utumizi wa lugha sanifu. Katika kiwango cha kisintaksia, usanifu wa ndani utahusisha matumizi ya miundo fulani ya sentensi, mfano sentensi sahili, changamano, matumizi ya virai n.k. Vigezo hivi huenda vitumiwe kudhihirisha ukiushi wa kisarufi wa kindani katika kiwango hiki.

Tutachanganua maswali ya undani ya kisarufi kama yanavyojitokeza katika jumbe cheshi. Tutaonyesha namna ukiushi wa kisintaksia unavyojitokeza katika mwelekeo huu. Mofolojia inahusisha muundo wa maneno. Pia, hushughulikia muundo wa ndani wa neno. Maneno hujengwa kwa mofimu. Kwa hivyo, mofolojia huhusisha maswala kuhusu aina tofauti za mofimu katika neno. Mofolojia hueleza mpangilio wa mofimu hizo katika neno na uhusiano wa mofimu zenyewe katika neno. Haya ni kwa mujibu wa Karanja na Habwe (2003). Ukiushi wa kimofolojia ni ukiukaji wa kimakusudi wa maswala yanayohusiana na neno kama vile kukiuka maendelezo sahihi ya neno, uundaji wa maneno wenye kukiuka sheria za uundaji, uambishaji usio sahihi miongoni mwa njia nyinginezo za ukiushi. Ukiushi wa kimofolojia unahusisha mvurugo wowote unaoweza kutendewa mofimu yoyote ya neno. Katika uchunguzi wetu, tutaonyesha namna ukiushi wa kimofolojia utakavyojitokeza katika jumbe maandishi za jumbe cheshi.

Katika kiwango cha kileksika, uleksika unahusisha uteuzi wa msamiati. Tutachanganua swala la misimu katika jumbe cheshi, matumizi ya lugha ng‟eni na kuchanganya misimbo. Ukiushi wa kileksika hufanywa kwa sababu za kiusanii na pia kwa malengo ya kufanikisha mawasiliano. Ukiushi wa kigrafolojia unahusu ukiushi wowote kwenye kaida za kimaandishi kama vile matumizi ya herufi kubwa kusikofaa. Ukiushi wa kigrafolojia unahusisha maandishi yasiyoheshimu mipaka ya neno, aya, matumizi ya sitiari za kigrafolojia kama vile kutumia rangi mahsusi kwa kusudi la kuzua maana fulani. Ukiushi huu pia huwezesha kuafikia mvuto fulani wa kiusanii kwenye kazi unapojitokeza.

Ukiushi wa kisemantiki unahusisha mahusiano ya maana yasiyolingana kimantiki na huzua ukinzani kwa kiwango fulani. Huhusisha aina tatu za ukiushi ambazo ni uhamishaji wa maana, uwongo wa kiusanii na pia uajabu wa kisemantiki. Tutachanganua jumbe cheshi katika kiwango cha ukiushi wa kisemantiki katika kiwango cha uhamishaji wa maana na kile cha uwongo wa kisanii. Kuna baadhi ya miundo ya kisemantiki ambayo haikubaliki na haiwezi kuzalishwa katika lugha ya Kiswahili.

**3.2 Ukiushi wa Kisintaksia katika Jumbe Cheshi**

Mawasiliano hayafanyiki kwa maneno tu bali huhusisha sentensi. Katika kufafanua haya, tutachanganua miundo tofauti ya sentensi zinazojitokeza kwenye jumbemaandishi za jumbe cheshi. Tutaonyesha jumbe cheshi zenye maandishi yanayokiuka sheria za utunzi wa sentensi katika Kiswahili sanifu. Tutaangazia aina tofauti za sentensi kimuundo, iwapo kuna vishazi au virai. Tutaonyesha namna swala la ukiushi wa kisintaksia linavyojitokeza kupitia miundo tofauti ya sentensi. Pia, tutachunguza aina tofauti za sentensi kiuamilifu; sentensi za maswali, amri, agizi n.k. Aina za sentensi zinazoonekana kujitokeza kwa wingi zitachukuliwa kama zenye ukiushi wa kiwango cha juu zaidi na kwa hivyo zitaangaziwa.

Aidha, swala la usambamba kama linavyojitokeza katika sentenzi litachanganuliwa. Usambamba utajitokeza kupitia mipangilio ya kiruwaza ya maneno au virai katika sentensi. Usambamba huwezesha mpangilio maalum wa mawazo, pia husaidia katika kufanya mawazo kukumbukika kwa urahisi. Wakati sentensi bila kukusudia inakuwa na muundo uliovurugwa na inakosa usambamba wowote hurejelewa kama yenye usambambamvurugo. Usambamba humwezesha mwandishi kufikia kiwango cha muwala. Wakati miundo ya sentensi haina usambamba, kazi ile husikika yenye kasoro na chapwa. Haya ni kwa mujibu wa Leech na Short (1981).


Katika kuchanganua kwetu, tutaweza kutumia jumla ya jumbe cheshi 49 kama data yetu ya kiuchunguzi. Jumbe cheshi hizi zitatumiwa kama ithibati katika kutolea mifano. Aidha, jumbe cheshi zingine zitatumiwa kama mifano kwenye vigezo tofauti. Kila jumbe cheshi itapewa nambari yake ya picha ya kuitambulisha. Jambo hili litarahisisha urejelezi wakati vigezo tofauti vinapofafanuliwa, pia litatusaidia kutorudiarudia jumbe cheshi moja kila mara inapotajwa kama mfano. Vilevile, katika uchanganuzi wetu wa jumbe cheshi kutoka kwa wavuti mbalimbali, tuliepuka kuchagua jumbe cheshi zisizozingatia tasfida katika maudhui yake, jumbe cheshi zinazoonyesha maswala ya ngono, jumbe cheshi zinazodhihirisha ukatili

kwa binadamu au wanyama, jumbe cheshi zinazoonyesha miegemeo mikali ya kisiasa na utubinafsi na pia jumbe cheshi zinazonuia kuibusha hisia za mshtuko au za kuogofya.

### 3.3 Ukiushi wa Kileksika wa Jumbe Cheshi

#### 3.0.1 Uhawilishaji Msimbo

Jumbe cheshi huonyesha uhamishaji ndimi wakati inapochanganya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine kwenye maandishi. Uhamishaji ndimi hadi kwa lugha ya kiingereza katika jumbe cheshi kunadhihirisha athari kubwa ambayo lugha ya Kiingereza inayo katika kizazi cha sasa.




Kuna mama uchi kwa gate.

**Picha 9: Uhawilishaji Msimbo**

#### 3.3.2 Kuchanganya Ndimi

Ni kuchanganya maneno machache ya lugha nyingine katikati ya sentensi ya lugha Kiswahili. Kwa mfano.




**Picha 10: Kuchanganya Ndimi**

#### 3.3.4 Matumizi ya Lugha Vipindi

Lugha vipindi ni lugha ambayo hubadilikabadilika. Lugha ya sheng kama lugha ya msimu inatumika kwa wingi. Lugha ya sheng‟ inatumika kwa wingi katika jumbe cheshi kwa sababu kwa kawaida hutumiwa na vijana ambao kwa kawaida ndio wenye kusambaza jumbe cheshi za mtandao kwa wingi.





Kukanyagia story kwa maana msiri au asiyesema mengi

**Picha 11: Matumizi ya Lugha Vipindi**

### 3.3.5 Matumizi ya Lafudhi

Lafudhi ni matamshi ya msemaji yanayotokana na athari za kimazingira kama vile lugha yao ya kwanza. Jumbe cheshi kutokana na ukweli kwamba zinaundwa ili kusambazwa kwa wasomaji wa makabila mengi hasa katika nchi ya Kenya hudhihirisha wingi wa matumizi lugha ya kilafudhi. Pia jumbe cheshi zinatumiwa kama njia ya kukejeli wazungumzaji wa maeneo fulani kwa namna wanavyosema lugha ya Kiswahili na athari za lugha zao za kwanza. Hii ni kwa sababu kila binadamu anayetumia lugha ya kuzungumzwa anayo lafudhi. mifano ya jumbe cheshi ni kama ifuatavyo.







Usiniletee Uchinga ya Nyeri pwana, hapa ni Kakamega pwana

Right choice sio joyce kwa maana alisema achaguliwe yeye katika uchaguzi sio mshindani wake anayeitwa Joyce. Msemaji ana lafudhi ya lugha ya Kikalenjin. Jumbe cheshi yenye menyu ya hoteli yenye lafudhi ya kikamba. Hapa ni Kakamega pwana badala ya bwana, hii ni lafudhi ya kiluhya.

**Picha 12 (a) (b) (c): Matumizi ya Lafudhi**

### 3.3.6 Utohozi

Kutohoa ni namna ya kuunda msamiati kwa kulifanya neno kutoka lugha nyingine likubaliane na kanuni za kifonolojia za lugha pokezi. Jumbe cheshi hutohoa maneno mengi hasa kutoka kwa lugha ya Kiingereza.Wakati mwingine utohozi huonekana kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kuzua ucheshi. Mfano




“Fulu” kwa maana ya “fool”: “Tuyu” kwa maana “to you”

**Picha 13: Utohozi**

### 3.3.7 Matumizi ya Lugha Bandya za Kisanaa.

Lugha ya jumbe cheshi kwa jumla inaonekana kukosa urasmi kwa vyovyote vile. Lugha bandya ni aina ya lugha inayonuiwa kuleta ujumi wa kisanaa katika mawasiliano yake kwa njia ya wavuti. Lugha hii inakusudiwa kudhihaki hali mbalimbali.

Mifano ya jumbe cheshi;




Buda na mtunguyaz

**Picha 14: Matumizi ya Lugha Bandya za Kisanaa**

### 3.3.8 Uumbaji Maumbo Mapya

Unahusisha uumbaji wa maneno hivi kwamba yanatumika kwa maana nyingine bali na ile iliyozoeleka katika Kiswahili sanifu. Mfano




**Picha ya 15; Uumbaji wa maumbo upya.**

Hapa neno “ameiva” lina maana ya “kuwa mrembo” au “kupendeza”.Maana hii inatofautiana na maana iliyozoeleka na ya kikamusi yenye maana ya chakula kuwa tayari baada ya kupikwa au hali ya tunda kukomaa na kuwa tayari kuliwa.

### 3.4 Ukiushi wa Kisintaksia katika Jumbe Cheshi

Maswala ya ukiushi wa kisintaksia na pia usambamba yanajitokeza kwa njia zifuatazo katika jumbe cheshi;

#### 3.4.1 Kishazi

Kishazi ni utungo au sentensi ambayo haiarifu kikamilifu hata ingawa ina kiima na kiarifu. Kuna vishazi tegemezi ambavyo haviwezi kujisimamia kutoa ujumbe kamili na vishazi huru ambavyo huarifu kiujumbe kama sentensi sahili. Jumbe cheshi nyingi zinaonyesha matumizi ya vishazi tegemezi ambavyo hutegemea kujalizwa na vishazi huru. Vishazi huru vya kujaliza ujumbe vinaonekana kuwa picha iliyoambatanishwa na ujumbe wa maandishi. Tazama mifano ifuatayo.






Mkisikia beshte yenu ameenda Nyeri ni utungokishazi. Sentensi inakamilishwa na fremu inayoonyesha wahusika wenye hisia za mshtuko.Ukiangusha 50bob ni utungo kishazi, sentensi inakamilishwa na fremu inayoonyesha watu wengi kuzitafuta hizo pesa.

**Picha 16 (a) na (b):  Matumizi ya Vishazi**

### 3.4.2 Matumizi ya Virai

Kirai ni sehemu ya sentensi ambayo huwa na neno kuu pamoja na maneno mengine yanayofafanua neno hili kuu. Kirai hakiarifu kama sentensi. Virai ni vya aina tofauti kulingana na muundo wake. Jumbe cheshi hudhihirisha matumizi ya virai ambavyo husimama kama sentensi ili kutoa ujumbe. Ujumbe kamili unatarajiwa kupatikana kutoka kwa picha iliyoambatana na kirai kile. Tazama mifano ifuatayo.







Wabunge wa Jamaica

Jamani wazima nyie

**Picha 17 (a) na (b):  Matumizi ya Virai**

### 3.4.3 Maswali ya Balagha

Jumbe cheshi hutumia miundo ya sentensi zenye maswali yasiyohitaji majibu. Maswali haya hayahitaji majibu bali yanalenga kuchochea hisia maalum kwa msomaji matinihusika. Hii ni kwa sababu ya kutilia mkazo ujumbe maalum kulingana na muktadha wa matumizi. Jumbe cheshi zingine hutumia sentensi zenye mubalagha.




Ni nani hawa wako kwako?

Nani amenitusi kwa group?

**Picha 18 (a) na (b): Maswali ya Balagha**

### 3.4.4. Kuboronga Maneno

Jumbe cheshi inapoboronga maneno huwa kwamba mpangilio wa maneno katika sentensi umevurugwa bila kukiuka kanuni za vipashio vya kisarufi kama vile ngeli.




Matumbo matumbo huumiza ngoja badala ya ngoja ngoja huumiza matumbo.

**Picha 19: Kuboronga Maneno**

### 3.4.4 Sarufi Mvurugo

Jumbe cheshi zingine zinaonekana kuvuruga kanuni za kisarufi za lugha ya Kiswahili kwa njia tofauti. Mvurugo unatokea katika matumizi yasiyo sahihi ya miundo ya ngeli kulingana na sarufi ya Kiswahili, upatanisho wa kisarufi usio sahihi wa vivumishi na nomino kwenye sentensi za jumbe miongoni mwa ukiushi mwingineo. Ukiushi huu unafanywa kama mtindo wa njia ya kuonyesha sifa za kisarufi za jumbe cheshi. Tazama mifano ifuatayo.




Mwenye umeleft

**Picha 20: Sarufi Mvurugo**

### 3.4.5 Matumizi ya Dayolojia

Jumbe maandishi kwenye jumbe cheshi zingine zinajitokeza kwa muundo wa dayolojia. Hii ni njia mojawapo ya kuonyesha wanaohusika katika mazungumzo pamoja na hisia za wahusika hao. Vilevile dayolojia husaidia kutuonyesha kwamba kuna uhalisia kwenye tukio linalohusika kwa sababu wahusika hufanywa kuongea kama waliomo katika hali yao halisi.




**Picha 21: Matumizi ya Dayolojia**

### 3.4.6 Usambamba wa Kisintaksia

Kama tulivyosema usambamba wa kisintaksia hujitokeza wakati ambapo kuna maumbo mawili au matatu kwenye sentensi yenye ruwaza au mpangilio wa kimuundo unaofanana. Katika jumbe cheshi, usambamba kwenye maumbo mbalimbali unajitokeza kwa namna zifuatazo.




KT(RT)+KT(RT)+KT(RT)+KT(RT); okoa jahazi, okoa bundles, okoa stima, okoa rent.

**Picha 22: Usambamba katika KT(RT)+KT(RT)+KT(RT)+KT(RT)**

Usambamba katika: KN1(N)+KT(T+N) +KN2(N)+KT(T+N); mapenzi ni pesa maua pelekea nyuki.




**Picha 23: Usambamba Katika KN1(N)+KT(T+N) +KN2(N)+KT (T+N)**

Usambamba Wa; KN1(W)+KT(T+N) +KN2(W)+KT(T+N)




mimi nikasema caanan; mimi nilisema tissue

**Picha 24:  Usambamba katika KN1(W)+KT(T+N) +KN2(W)+KT(T+N)**

### 3.4.7 Usambamba Kinyume

Huu ni ukiushi ambapo matamko yenye maana kinyume, yaani ya kiantonimu huwekwa pamoja ili kukamilishana kimaana. Ukiushi huu huwa na lengo la kuonyesha ubunifu wa mtunzi au mwandishi. Mifano hii ya jumbe cheshi inaonyesha ukiushi huu.




Chezea ujana uzee ni finals; ujana ni antonimu ya uzee
Mtoto akisikia kuna pesa ya wazee; mtoto ni antonimu ya waliozeeka yaani wazee.

**Picha 25: Usambamba Kinyume**

### 3.4.8 Usambamba Kimwimo

Kimwimo ni dhana inayorejelea namna ishara za lugha zinavyohusiana kiwima. Ferdinard de Saussure katika kufafanua nadharia ya sarufi miundo alieleza aina mbili za mahusiano ya

ishara katika sentensi. Kwamba kuna uhusiano kimwimo na uhusiano kimlalo. Mahusiano kimlalo hueleza namna ishara za lugha zinavyofuatana moja baada ya nyingine kimraba. Mahusiano kimwimo huchanganua mahusiano ya ishara za lugha kiwima katika muktadha maalum. Mahusiano wima yanaonyesha usambamba kwa namna maneno yanavyohusiana kutoka juu kwenda chini kwenye jumbe cheshi ifuatayo ambapo kimuundo, maneno yamepangwa mawili mawili kiwima na maneno yenyewe ni kategoria sawa za muundo aina ya vitenzi katika kila orodha.

Unaniringia(T)

Hujui(T)

Huniita(T)





**Picha 26: Usambamba Kimwimo**

### 3.5 Ukiushi wa kimofolojia

Ukiushi wa kimofolojia utajitokeza kwa njia zifuatazo katika jumbe cheshi;

#### 3.5.1 Ukatizaji

Ni mbinu ya kufupisha maneno ili yawe na silabi chache kuliko yale asilia. Kwa kawaida mbinu hii hutumika zaidi katika lugha ya mazungumzo na kwa hivyo inapotumika katika maandishi, itarejelewa kama ukiushi.




Ka si malaria

**Picha 27: Ukatizaji**

### 3.5.2 Uambishaji

Jumbe cheshi zingine zina viambishi vilivyodondoshwa. Zingine zimeongezewa viambishi kwa namna ilivyokiuka uambishaji sahihi wa maneno katika sarufi ya Kiswahili.




Jamaneni badala ya jamani viambishi [ne][ni] vimeongezewa kwenye neno.

**Picha 28: Uambishaji**

### 3.5.3 Mnyambuliko

Jumbe cheshi zingine zinaonyesha minyambuliko iliyokiuka kanuni za mnyambuliko kwa kutotumia alomofu zifaazo katika kunyambua maneno yake.




Hawachatingi badala ya hawachati

Unazindikishwa badala ya unasindikizwa

**Picha namba 29  Ukiushi wa  Kunyambua**

### 3.5.5 Ukiushi Kitahajia

Jumbe maandishi zingine katika jumbe cheshi zinakiuka sheria ya kitahajia kwenye baadhi ya maneno kwenye jumbe. Ukiushi wa kitahajia unatokea wakati mipaka ya neno haiheshimiwi na kwa hivyo maneno mengine yanajitokeza yakiwa mawili wakati ambapo linafaa kuwa neno moja pekee. Mengine yameongezewa sauti au kuzibadilisha sauti fulani katika maneno ambazo hazistahili kuwepo. Maneno mengine yanasomeka kama neno moja ilhali idadi yake imezidi moja.








Walio olewa badala ya walioolewa

Washa badala ya wacha

**Picha 30 (a) na (b): Kitahajia**

### 3.5.6 Kuchanganya Maumbo

Jumbe zinahusisha maumbo kutoka lugha ya Kiingereza yanayoambatanishwa na maumbo ya lugha ya Kiswahili ili kuunda neno moja. Kuchanganya maumbo hurahisisha kueleweka kwa ujumbe haraka.




Ali-confuse

**Picha 31: Kuchanganya Maumbo**

### 3.5.7 Usambamba wa Kimofolojia

Jumbe cheshi zingine zina maneno yenye miundo inayojirudiarudia kwenye sehemu maalum kwenye maneno husika. Usambamba wowote kwa kawaida hufanyika ili kuongezea mvuto wa kiusanii kwenye utungo husika.




Waluhya [wa] waliposikia [ wa]

Akabeba sadaka akahepa [a][ka]

**Picha 32 (a) na (b): Usambamba wa Kimofolojia**

## SURA YA NNE

## UKIUSHI WA KISAJILI

### 4.0 Utangulizi

Kigezo kikuu cha ukiushi wa kisajili ni kuchanganya sajili katika matini moja. Kwa kuchanganya sajili, ucheshi wa kiisimu huafikiwa. Mifano ifuatayo itatumiwa kudhihirisha hayo katika jumbe jumbe cheshi:

(a) Sajili ya kisheria na sajili ya kiteknolojia zimetumiwa pamoja katika kuchanganua maswala ya kijamii katika mfano ufuatao wa jumbe cheshi.




"Server yake" ni neno katika sajili ya kiteknolojia. "34b" ni neno kutoka sajili ya kisheria inayorejelea aina maalum ya fomu inayotumiwa kurekodi idadi mahsusi ya kura zilizohesabiwa katika kituo fulani cha upigaji kura kulingana na sheria katika nchi ya Kenya. Swala la kijamii linalorejelewa ni kuhusu baba aliyemzaa mtoto.

**Picha 33: Ukiushi wa Kisajili**

(b) Sajili ya kibiashara kuingizwa ili kuelezea maswala ya kisiasa;




"Tissue ni Hanaan" ni tamko kutoka sajili ya matangazo ya kibiashara. "Caanan" ni tamko lililotumika na chama fulani cha kisiasa nchini Kenya katika uchaguzi mwaka 2017. Chama hicho pinzani kiliwaahidi wafuasi wake maendeleo na mambo mazuri kama

ya nchi ya Caanan katika Bibilia iwapo kingepata ushindi. Kiliposhindwa katika kura, wanachama walishtuka kwa kuwa hawakupelekwa Caanan. Tashtiti inadokeza walivyopatwa na mshtuko kwa kushindwa katika uchaguzi hadi wakaugua maradhi ya tumbo.

**Picha 34: Sajili ya Kibiashara na Siasa**

(c) Sajili ya kidini kutumiwa katika mawasiliano ya simu kama inavyojitokeza.




Neno "umelaaniwa" kwa kawaida hutumika katika sajili ya kidini. Fremu ya jumbe cheshi inaonyesha mtu aliyebeba Bibilia na aliyevalia mapambo yenye ishara za kidini. Ujumbe hauhusu maswala ya kidini bali unarejelea maswala ya kimawasiliano hasa wanaoondoka kutoka vikundimawasiliano bila sababu. Jambo hili linakusudiwa kuzua ucheshi ambao ni sifa kuu ya jumbe cheshi.

**Picha 35: Sajili ya kidini**

(d) Sajili ya darasani kutumiwa kuelezea maswala ya kisiasa kama ifuatayo;




Fremu inaonyesha mwalimu Wanjiku anayeigiza kuwa mwalimu wa somo la Kiswahili darasani. Wanasiasa kutoka nchi ya Kenya wanaonekana kufanya makosa ya lugha kama mwalimu Wanjiku anavyofanya. Jumbe cheshi hii inakusudia kuzua ucheshi wa kinaya

kwamba wanaotarajiwa kuzingatia lugha sahihi kama walimu na wanasiasa wako mstari wa mbele katika kuharibu lugha sanifu.

**Picha 36: Sajili ya darasani kutumiwa kuelezea maswala ya kisiasa**

(d) Sajili ya kiutawala inatumiwa kuelezea maswala ya kijamii kama ifuatavyo.




Tamko lililoko katika jumbe cheshi hii hutumiwa katika maswala yanayohusisha rais katika mikutano ya kitaifa nchini Kenya. Swala la kijamii linalorejelewa ni kuhusu mfumko wa bei za bidhaa; tamko hili linazua tashtiti linapotumiwa kuelezea maswala ya uchumi ulivyo mgumu kwa wananchi kwa njia inayozua ucheshi.

**Picha 37: Sajili ya kiutawala inatumiwa kuelezea maswala ya kijamii**

(f) Sajili ya vijana inatumiwa katika maongezi ya mzee.




Kwa kawaida, vijana ndio watumizi wa mtandao na hujiunga na vikundi mawasiliano tofauti katika mitandao. Pia, kwa kawaida vijana humiliki vifaa vya kimawasiliano kama

vile simu, vipakatalishi au kompyuta. Anayehusika katika shughuli ya kimawasiliano kulingana na fremu ni mzee anayeonekana kushiriki katika mawasiliano ya vikundimawasiliano jambo ambalo si kawaida. Ucheshi huu unalenga kuonyesha namna teknolojia ilivyoathiri kila mmoja katika jamii; wazee hata vijana.

**Picha 38 Sajili ya Vijana inatumiwa katika Maongezi ya Mzee**

## 4.1 Ukiushi wa Kigrafolojia.

Ukiushi wa kigrafolojia hujitokeza kwa njia zifuatazo katika jumbe cheshi.

(a) Kutambulisha maana kwa matumizi ya rangi za kitaashira kwenye jumbe zinazojitokeza kama sitiari za grafolojia. Kwa mfano, maandishi katika jumbe cheshi ifuatayo yamewekwa katika rangi nyekundu kuleta maana kuwa yanayowasilishwa hayazui hisia za furaha. Rangi nyekundu itahusishwa na hisia hizi kutokana na imani za kitamaduni zinazohusishwa na rangi hiyo.




"Huyu atamaliza shule kweli" swali hili linazua hisia zenye wasiwasi kwani mtoto katika fremu anaonekana kuwa na utovu wa nidhamu. Picha hii nyingine inaeleza maswala ya kuzingatia usafi kwa njia yenye ucheshi

**Picha 39 (a) na (b): Ukiushi wa Kigrafolojia.**

(b) Kuwepo au kutokuwepo kwa alama mbalimbali za uakifishaji ili kuzua maana zinazokusudiwa kama ifuatavyo.




Chai kila saa, pika chapati, toa hio kipindi…

**Picha 40: Matumizi ya Alama za Dukuduku**

ii) Matumizi ya herufi kubwa na ndogo kama ifutavyo.




Maneno muhimu yamewekwa katika herufi kubwa ili kutoa msisitizo wa ujumbe muhimu kuwa kwa walioolewa simu hukutoza machozi.

**Picha 41: Matumizi ya Herufi Kubwa na Ndogo**

(iii) Alama ya kinyota kuleta maana ya mambo yenye umarufuku au mwiko kama ifuatavyo kwenye jumbe cheshi.




Jina “nasa” ni marufuku kwa upande wa serikali kwa sababu ni jina la chama pinzani. Alama hii inatumiwa kuonyesha hisia za kisiasa katika nchi ya Kenya.

**Picha 42: Alama ya Kinyota kuleta maana ya Mambo yenye Umarufuku**

(iv)) Maandishi yanayodhihiri maana kulingana na sehemu yaliyowekwa kwenye fremu.




Maandishi yaliyowekwa upande wa chini wa fremu yanaonekana kuwa majibu ya maandishi yaliyo kwenye upande wa juu wa fremu. Hali inayojitokeza ni kuwa upande wa juu na wa chini zinaonekana kuwasiliana kama wahusika wawili tofauti.Out sio lazima beach…bali ni popote patulivu

**Picha 43: Maandishi yanayodhihiri maana kulingana na Sehemu Yalikowekwa**

(v)) Kundi la jumbe cheshi kadha katika ukurasa mmoja wa picha zikitumiwa kwa pamoja kama fremu moja kuelezea wazo moja kama ifuatavyo.




Wazo kuu katika jumbe cheshi ifuatayo ni kuhusu mapuuza ya wanajamii mbalimbali katika kuzingatia Kiswahili sanifu katika mawasiliano yao.

**Picha 44: Kundi la Jumbe Cheshi Kadha katika Ukurasa Mmoja**

**(vi) Kutoakifisha sentensi**

Sentensi zingine zinatumia herufi ndogo kwenye mianzo yake. Pia zinapofikia tamati hazitiwi nukta kuashiria kuhitimishwa kama ifuatavyo. Jumbe cheshi ifuatayo haijaanza kwa herufi kubwa na pia alama ya kiulizo inakosekana. Herufi ndogo inatumiwa kuanza kudokeza hisia za taharuki, Pia sentensi yenyewe inasikika ikiwa swali hata ingawa alama inakosekana.




atamaliza shule huyu[?]

**Picha 45: Kutoakifisha Sentensi**

### 4.2 Ukiushi wa Kisemantiki

Ukiushi wa kisemantiki katika jumbe cheshi unajitokeza kwa njia mbili kuu ambazo ni uhamishaji wa maana na pia uwongo wa kisanii. Njia kuu za uhamishaji maana ni kupitia matumizi ya sitiari, metonimu na matumizi ya tashbihi.

#### (a) Matumizi ya Sitiari

Sitiari ni mbinu ya ulinganisho kwa matumizi ya vitu visivyohusiana kwa kawaida. Sitiari huwa na sehemu mbili ambazo ni dhana kuu na pia picha inayowasilishwa. Sitiari huwa na umuhimu wa kueleza dhana kwa njia wazi, hufanya maana kueleweka kwa njia wazi. Aidha, husaidia katika kupamba lugha. Mfano wa sitiari ni kama ifuatavyo katika jumbe cheshi.




Mapenzi ni pesa kwa maana bila pesa mapenzi hayazui furaha.

**Picha 46: Matumizi ya Sitiari**

#### (b) Matumizi ya Tashbihi

Huu ni ulinganisho unaolazimisha vitu viwili kufanana hata kama havina uhusiano katika hali halisi.



Simu ya mwanamume ni kama kitunguumaji. Tashbihi hii inatumiwa kusisitiza ujumbe uliopo na pia kuipamba lugha iliyopo.

**Picha 47: Matumizi ya Tashbihi**

**(c) Matumizi ya Chuku**

Chuku ni mbinu ya kutilia chumvi habari iliyopo ili kutilia mkazo dhana yenyewe. Chuku hueleza mambo kwa njia iliyokithiri viwango vya juu vya kutia chumvi kama ifuatavyo.




Kwamba kuchanga shilingi elfu moja husababisha mtu kufuatwa na wanawake wanaotaka kuolewa.

**Picha 48: Matumizi ya Chuku**

**(d) Matumizi ya Kinaya**

Kinaya ni usemi ambao kwa kawaida huibuka kama kinyume cha matarajio. Matarajio ya mwandishi anapotumia kinaya ni kwamba msomaji atatambua maana kwa namna inavyokusudiwa. Kinaya kimejitokeza kwa njia zifuatazo katika jumbe cheshi.






Ni kinaya kwamba ngombe mkosa afya anasemekana kutoa maziwa mengi sana. Ni kinaya kwamba atalala njaa hata baada ya kula chakula aina kingi.

**Picha 49 (a) na (b): Matumizi ya Kinaya**

# SURA YA TANO
# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Ni wazi kuwa jumbe cheshi za mtandao zinaonyesha ukiushi wa kiisimu katika viwango tofauti vya kiisimu. Tuna uhakika kuwa walioziona jumbe cheshi kama zenye kubeba aina mbalimbali ya makosa wameanza kuziona jumbe cheshi kwa mwelekeo mwingine tofauti.Tulikusudia kuonyesha kuwa makosa yaliyopo kwenye jumbe husika huwa ni ya kimakusudi na hulenga kuzua mvuto fulani wa kiusanii. Aidha, kupitia nadharia ya semiotiki, jumbe cheshi zitachukuliwa kama ishara zenye maana tofautitofauti. Ishara hizi zenye maana zinaweza kutumiwa katika ulimwengu wa sasa katika nyanja mbalimbali kama vile katika kuunda matangazo ya kibiashara. Jumbe cheshi zinaweza pia kutumiwa na wanajamii mbalimbali kupitisha hisia zao. Pia, jumbe cheshi ni kifaa cha burudani na kwa hivyo zinaweza kutumiwa kupitisha wakati na kujipumbaza.

Katika uchanganuzi wetu, tulikumbana na jumbe cheshi zenye jumbe tofautitofauti. Zingine zilikuwa zenye miegemeo mikali sana ya kisiasa hususan katika kueleza maswala ya kisiasa katika nchi ya Kenya hasa mambo yanayohusiana na uchaguzi nchini. Jumbe cheshi zingine zilikosa lugha yenye tasfida. Kunazo zenye utubinafsi mwingi kuhusiana na maswala tofauti ya kijamii. Jumbe cheshi hizo tuliweza kuzipuuza katika uchanganuzi wa data yetu ya utafiti. Hii ina maana kuwa hata ingawa jumbe cheshi ni zenye umuhimu kama tulivyotaja hapo juu, wakati mwingine zinaweza kutumiwa kuleta migawanyiko katika jamii na vilevile kudidimiza maadili hasa miongoni mwa vijana ambao ndio idadi kubwa ya watumizi mtandao.

## 5.1 Muhtasari

Utafiti wetu ulilenga kuonyesha ukiushi wa kiisimu wa jumbe cheshi za mtandao katika viwango sita vya kiisimu. Ulilenga kutatua tatizo letu lililoko katika sura ya kwanza kwamba jumbe cheshi za mtandao huwa zenye kukiuka sarufi sanifu ya lugha ya Kiswahili kwa kudhihirisha makosa ya kila sampuli yanayoonekana kukiuka sarufi na kanuni za lugha ya Kiswahili. Tumefaulu kuonyesha kuwa kinachoonekana kama makosa ya lugha ni dhana ya kimakusudi inayohusisha kuunda mvuto wa kiusanii kwa msomaji wa jumbe cheshi kupitia ukiushi wa kiisimu katika viwango sita kama inavyodhihirika katika sura ya tatu na ya nne. Malengo yetu matano kama tulivyoyafafanua katika sura ya kwanza yameweza kuafikiwa. Nadharia ya semiotiki imetuelekeza katika kueleza jumbe cheshi kama ishara ambazo

hubeba maana mbalimbali. Nadharia ya elimumitindo ilitumiwa katika kueleza namna ukiushi mbalimbali wa kiisimu unavyojitokeza kwenye jumbe cheshi katika viwango sita vya kiisimu.

Katika sura ya pili, tumeonyesha muundo wa jumbe cheshi kinadharia na kuonyesha aina mbalimbali za jumbe cheshi hasa za kidijitali. Sura hii ililenga kuonyesha jumbe cheshi ni nini kwa uwazi zaidi kwa kuwa jumbe cheshi hizi ndizo data yetu kuu ya utafiti. Katika sura hii tumeonyesha miundo ya jumbe cheshi pamoja na maswala yanayojitokeza katika jumbe cheshi kwa kurejelea aina yake.

Katika sura ya tatu, tulionyesha namna jumbe cheshi zinavyodhihirisha ukiushi wa kisarufi uliohusisha uchanganuzi wa maswala ya kisintaksia na kimofolojia. Ukiushi wa kisintaksia ulihusu kuonyesha dhana tofauti za ukiushi zinazojitokeza katika kiwango cha sentensi. Ukiushi wa kimofolojia ulihusisha kuonyesha mivurugo aina tofauti inayojitokeza katika miundo ya maneno ya jumbe cheshi husika. Ukiushi wa kileksika ulijadiliwa katika sura hii pia. Maswala ya kileksika yaliyofafanuliwa yalihusisha uundaji wa maumbo mapya ya maneno kwa njia tofautitofauti.

Sura ya nne nayo ilijadili ukiushi wa kisajili ambapo maswala mbalimbali ya kisajili yanajitokeza kama dhana za ukiushi. Tumejadili pia ukiushi katika kiwango cha kigrafolojia ambao ulihusisha kuonyesha miundo mbalimbali ya kimaandishi kama vigezo vya ukiushi. Vilevile ukiushi wa kisemantiki umejadiliwa katika viwango viwili ambavyo ni uwongo wa kiusanii na uhamishaji maana.

## 5.2 Changamoto katika Utafiti

Changamoto tulizokumbana nazo hasa zilihusisha wavuti mbalimbali ambazo zilikuwa kiini cha data yetu ya uchunguzi. Changamoto ya kwanza ni kuwa jumbe cheshi zenye maandishi katika lugha ya Kiswahili ni chache sana tukilinganisha na jumbe cheshi katika lugha nyingine kwa mfano lugha ya Kiingereza. Kunazo Wavuti chache sana zinazojihusisha na jumbe cheshi katika lugha ya Kiswahili. Changamoto ya pili inahusu sifa kuu ya jumbe cheshi nyingi kwamba hazidumu kwenye mtandao. Hizi ni aina tulizorejelea kama jumbe cheshi tangazi. Tuligundua kuwa kila siku jumbe cheshi mpya zilijitokeza kuzungumzia maswala tofauti yaliyoibuka katika jamii. Jumbe cheshi zingine zilionekana kupotea baada ya kipindi kifupi tu. Pia zingine zilijibadilisha kimaandishi huku fremu zikibaki zilezile baada ya kuundwa upya. Kukosa udhabiti huku kwa jumbe cheshi hizi kulizua changamoto fulani katika kupata data isiyobadilikabadilika. Changamoto nyingine ilihusiana na sifa za jumbe

cheshi nyingine kukosa tafsida na pia kuwa na miegemeo mikali ya kisiasa miongoni mwa mengineyo. Hii ilikuwa changamoto kwetu kwa kuwa tulipata jumbe cheshi nyingi sana kiidadi kutoka kwa mtandao lakini tungeweza kutumia chache tu ambazo zilikuwa na sifa tulizohitaji. Jambo hili pia lilisababisha kuchukua siku nyingi ili kutafuta jumbe cheshi tulizohitaji kama data ya uchunguzi.

Jumbe cheshi kama chombo cha mtandao kinachosambazwa kwa kasi na kwa watu wengi inaweza kufana sana iwapo itatumiwa na wanajamii mbalimbali katika kusambaza mambo muhimu. Mambo haya muhimu ni kama vile zitumiwe katika kufunza maswala mbalimbali kama vile ya kielimu mintarafu lugha. Pia jumbe cheshi zinaweza kutumiwa kama vyombo vya kufanya matangazo ya kibiashara ya bidhaa na huduma mbalimbali. Aidha, kwa kuwa jumbe cheshi zinahusiana na ubongo wa msomaji, maoni yangu ni kuwa zinaweza kutumiwa katika kitengo cha matibabu kuwatibu wagonjwa wenye machovu ya akili ili kuwatuliza kiakili wanaposoma jumbe cheshi tofauti zenye ucheshi.

Ni muhimu kutaja kuwa kikwazo mojawapo kuhusiana na matumizi yenye faida ya jumbe cheshi ni matumizi ya lugha katika jumbe cheshi isiyozingatia tasfida. Vilevile, jumbe cheshi zingine zinadidimiza maadili kwa kusambaza maswala ya ngono miongoni mwa vijana. Jumbe cheshi zingine husambaza kauli za uwongo miongoni mwa wanajamii. Zingine hasa za kisiasa huonyesha miegemeo mikali ya kisiasa na hulenga kuwavua nguo washindani wa kisiasa kwa kueneza uvumi kuwahusu. Serikali kupitia taasisi zinazohusika na mawasiliano kupitia mtandao inafaa kuchukua hatua ili kusitisha matumizi yasiyofaa ya jumbe cheshi yanoyokiuka maadili tofauti ya kijamii.

### 5.3 Mapendekezo

Utafiti wetu ulilenga kuonyesha ukiushi wa kiisimu katika jumbe cheshi za mtandao. Maswala mengine mengi yanayohusu jumbe cheshi yanaweza kuchanganuliwa. Uchanganuzi wa kina kuhusu aina tofauti za makosa kama yanavyojitokeza katika jumbe cheshi unaweza kufanywa. Vilevile, jumbe cheshi zinahusisha jumbe maandishi pamoja na fremu za jumbe cheshi husika. Uchanganuzi unaweza kufanywa ili kueleza mahusiano tofauti ya kisemantiki yaliyopo baina ya fremu na jumbe maandishi zilizopo. Aidha, uchanganuzi wa jumbe cheshi unaweza kufanywa kwa kuzingatia mielekeo mingine tofauti kinadharia.

## MAREJELEO


Bally, C. (1916). *A Course in General Linguistics*. Columbia University Press.

Barthes, R. (1981). *Theory of the Text.* Ian Macleod katika R. Young. London: Edward Arnold

Blackmore, S. (2001). *The Meme Machine*. Oxford University Press, New York.

Burt, M na Kiparsky, C. (1972). *The Gooficon: A repair manual for English*. Rowley: Newbury House.

Chapman, R. (1973). *Linguistics and Literature: An Introduction to Literary Stylistics*. London: Edward Arnold.

Danesi, M. (2003). *Understanding Media Semiotics*. New York: Oxford University Press.

Dawkins, R. (2006). *The Selfish Gene*. Oxford University Press, New York.

Ferdinand de Saussure. *Aaccentuation lituanienne.* In: Indogermanische Forschungen. Vol. 6, pp 157 – 166.

Fish, S. (1980). *Is There A Text in This Class?: The Authority of Interpretive communicaties*. Harvard University Press.

Fowler, R. (1973). *Style and Structure in literature: Essays in the New stylistics.* Cornell University Press.

Freeman, D.C. (1970). *Essays In modern stylistics*. London: Methue.

Gil, P. (2016). Work source: https://www.lifewire.com/what-is-a-meme-2483702.

Habwe, J. & Karanja, P. (2003). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Halliday, M.A.K & Strevens, P. (1964). *The Linguistic Sciences and language Teaching*. London; Longmans Green and co.ltd.

Halliday, M.A.K. (1978). *Language as a Social Semiotic*. London; Edward Alnold.

Kövecses, Z. (2006). *Language, mind, and culture*: A practical introduction. Oxford and NewYork: Oxford University Press

Kovecses, Z. (2015). *Where Metaphors come from*. Oxford University Press. New York.

Leech, G.N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*.London; Longman.

Leech, G. and Short, M. (1981). *Style in Fiction*: *A linguistic Introduction to English Fictional Prose*. London/New York, Longman.

Aronoff, M. & Rees-Miller, J. (2008). *The Handbook of Linguistics*. John Wiley & Sons, p. 96.

Mcintosh (1960). *Graphology and Meaning. Glassgow*: republished in M.A.K. Halliday, A. Macintosh. *Patterns of language*: London.

Miall, D.S. and Kuiken, D. (1994). *Foregrounding, Defamiliarization, and Affect Response to Literary Stories*. University of Alberta.Elsevier Science B.V.

Mukarovsky, J. (1964). *Standard Language and Poetic Language*. Washngton. D.C; Georgetown University Press.

Pierce, C.S. (1991). *Peirce on Signs.* (Edited by Hoopes, J.) University of Carolina Press; Chapel Hill and London.

Riffatere, M. (1959). *Criteria for Style Analysis*.WORD; pp 154-174.

Shifman, L. (2013). Memes in a Digital World: Reconciling with a conceptual Troublemaker" *Journal of computer-Mediated Communication.*

Sitaram, A. and Bernardo, H. (2010). Jarida la Predicting the Future with Social Media. *https://arxiv.org/pdf/1003.5699*

Thornborrow, J. and Wareing, S. (1998). Patterns in Language: *An introduction to language and literary style*. Psychology Press.

Spitzer, L. (1967). *Linguistics and Literary History*. Princeton University Press.

Minium, Edward W. (1978). Statistical *Reasoning in Psychology and Education*. 2nd ed. John Wiley & Sons, NY.

Yebonah, P. & Dominic, M. (2014). Jarida la Education and Practice; *The Impact of Whatsapp Messenger Usage on Students Performance in Tertiary Institutions in Ghana*; Vol 5(6). www.iiste.org>…>Yeboah. Youth village.co.ke.